

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI
IDARA YA KISWAHILI**

**UCHANGANUZI WA MAKOSA YANAYOFANYWA NA WANAFUNZI
WAZUNGUMZAJI WA LUGHA YA EKEGUSII**

JANE MORAA OBARA – C50/75716/2012

WASIMAMIZI

DKT. PRISCA JERONO

BW. B. G. MUNGANIA

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Nairobi.

(2014)

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijatolewa popote ili kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Sahihi_____

Tarehe_____

Jane Mora Obara

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.

Sahihi_____

Tarehe_____

Dkt. Prisca Jerono

(Msimamizi)

Sahihi_____

Tarehe_____

Bw. B.G. Mungania

(Msimamizi)

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mume wangu mpendwa Daniel ambaye kwa uvumulivu mwingi alishirikiana nami kugharamia masomo yangu. Pia naitabarukia marehemu mamangu Mary Kerubo aliyenilea na kunihimiza kusoma hadi kiwango cha juu zaidi. “Mama! Ungeishi uone matunda ya jitihada zako.” Hatimaye namkumbuka binti yangu Mary aliyenivumilia na kunipa sababu ya kujitolea kwa bidii.

SHUKRANI

Ningependa kuwashukuru nyote mliochangia katika ufanisi wa kazi hii yangu. Kwanza kabisa namshukuru Mola kwa kunijalia afya na uwezo wa kupata shahada hii ya uzamili. Ameniongoza katika safari hii ndefu na kunijalia kutimiza ndoto yangu ya miaka mmingi ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa mchango wao walionipa. Nawashukuru wahadhiri wafuatao : Prof. Kineene, Prof. Habwe, Bw. Mungania, Prof. Mbatiah, Dkt. Zaja, Dkt. Mbuthia, Dkt. Iribemwangi, Dkt. Swaleh na Dkt. Jefwa. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Bw. Mungania na Dkt. Jerono. Nawashukuru sana kwa ushauri wao wa kitaaluma na zaidi ya yote kwa kunielekeza, hasa pale nilipoonekana kukosa mwelekeo. Nayathamini sana maelekezi yao ambayo kwayo ndiyo sababu ya ufanisi wa kazi hii.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu tuliokuwa pamoja katika safari hii. Wanafunzi hawa ni : Grace, Ruth, Magdalene, Jael, Vincent, Regina, Sis. Teresia, Julius, Beatrice, Mariam, Furaha, Samwel, Duncan, Scholar, Doris, Nahashon, Margret K. na Margret M. Wote hawa tulikuwa abiria katika chombo kimoja na tulihimizana kuendelea na safari japo ilionekana kuwa ngumu. Namshukuru sana Ruth, kwa kunipa motisha na msukumo wa kuniwezesha kufanikisha kazi hii.

Ningependa kumshukuru mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Ekenyoro, aliyenihimiza kuendelea na masomo yangu na kunipa fursa mwafaka ya kufanya utafiti huu. Aidha alinikubalia kupata data kutoka shulen humo. Pia nawashukuru walimu wote wa shule hii kwa kunipa moyo na kunitakia heri na fanaka katika juhud zangu. Namshukuru pia mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Rirumi kwa kunikubalia kupata data kutoka shule yake.

Namshukuru kwa moyo wa dhati mume wangu kwa uvumilivu wake nilipokuwa masomoni. Aligharamia masomo yangu pamoja na mahitaji mengine. Bila msaada wake nisingeweza kuubeba mzigo huu pekee yangu. Alinitia moyo na kunihimiza kila mara kwa kweli alikuwa mwenza aliyenijali na kunifaa kwa mengi. Namshukuru pia binti yangu aliyevumilia upweke wakati sikuwepo. Anihimiza kufanya bidii niwe nambari moja. Kwa kweli mlinionyesha mapenzi yasiyo kifani.

Kwenu nyote mlioshiriki kufanikisha kazi hii nawashukuru sana na Mungu awabariki.
Ahsanteni.

IKISIRI

Madhumuni ya utafiti huu ni kuchanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii. Utafiti huu ultathmini ni kwa kiwango kipi lugha ya Ekegusii inachangia makosa hayo. Ili kufikia malengo ya utafiti huu, wanafunzi kutoka viwango viwili tofauti vyatya usomi waliandika insha ambazo zilisahihishwa na makosa yaliyopatikana kuchanganuliwa kwa misingi ya mtazamo wa Uchanganuzi Makosa. Makosa hayo yaliainishwa katika kategoria mbalimbali kisha sababu zinazosababisha makosa hayo kuelezw. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwepo kwa makosa haya katika viwango vyote japo kadiri mwanafunzi anavyoendelea na masomo katika viwango vyatya juu, makosa yanapungua. Lugha ya Ekegusii ilichangia pakubwa kutokea kwa makosa haya.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA	xi
MAELEZO YA DHANA ZILIZOTUMIWA	xi
SURA YA KWANZA.....	1
1.1 Usuli wa mada.....	1
1.2 Tatizo la utafiti	2
1.3 Madhumuni ya Utafiti	5
1.4 Nadharia tete	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada Hii.....	6
1.6 Upeo na Mipaka	7
1.7 Msingi wa Kinadharia	8
1.7.1 Lughha Kadirifu	9
1.7.2 Uchanganuzi Makosa	10
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu somo hili	12
1.9 Mbinu za Utafiti	17
1.9.1Mbinu za kukusanya data.....	16

1.9.2 Mbinu za kuchanganulia data.....	16
1.10 Umuhimu wa Utafiti.....	17
 SURA YA PILI.....	18
2.0 FONIMU NA SILABI ZA KISWAHILI SANIFU NA EKEGUSII	18
2.1 Utangulizi.....	18
2. 2 Fonimu za Kiswahili sanifu	19
2.3 Fonimu za Ekegusii.....	20
2.3.1 Fonimu za irabu za Ekegusii.....	20
2.3.2 Konsonanti za Ekegusii	22
2.4 SILABI ZA KISWAHILI SANIFU NA EKEGUSII.....	27
2.4.1 Muundo wa Silabi katika Kiswahili sanifu.....	28
2.4.1.1 Muundo wa silabi pendwa (KI).....	28
2.4.1.2 Muundo wa konsonati konsonati irabu(KKI)	28
2.4.1.3Muundo wa konsonanti kiyeyusho irabu (KYI).....	29
2.4.1.4 Muundo wa konsonanti konsonanti kiyeyusho irabu (KKYI)	29
2.4.1.5 Muundo wa irabu pekee (I).....	29
2.4.1.6 Muundo wa konsonanti pekee (K)	29
2.4.1.7 Muundo wa konsonanti irabu irabu (KII)	30
2.4.1.8 Silabi fungo	30
2.4.1.9 Muundo wa konsonanti konsonanti konsonanti irabu	30
2.4.2Muundo wa silabi katika lugha ya Ekegusii	31
2.4.2.1 Muundo wa konsonanti irabu (KI)	31
2.4.2.3 Muundo wa konsonanti konsonanti irabu (KKI).....	32

2.4.2.4 Muundo wa konsonanti kiyeyusho irabu (KYI).....	32
2.4.2.5 Muundo wa irabu pekee (I).....	33
2.4.2.6 Muundo wa konsonanti irabu irabu(KII)	33
2.4.3 Ulinganuzi wa miundo ya silabi za Kiswahili sanifu na Ekegusii	34
2.5 Hitimisho	35
 SURA YA TATU	36
3.0 UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KISINTAKSIA.....	36
3.1 Utangulizi	36
3.2 Makosa ya kifonolojia	37
3.2.1 Matumizi ya /r/ badala ya /l/.....	38
3.2.2 Matumizi ya /ʃ/ badala ya /ç/	39
3.2.3 Matumizi ya /s/ badala ya /z/	40
3.2.4 Matumizi ya /s/ badala ya /ʃ/.....	40
3.2.5 Matumizi ya /p/ badala ya /b/.....	41
3.2.6 Matumizi ya /b/ badala ya /p/.....	41
 3.3 Makosa ya Kimofolojia.....	42 <u>2</u>
3.3.1 Uchopekaji wa irabu /u/.....	43
3.3.2 Udondoshaji wa sauti /h/	43
3.3.3 Uyeyushaji	45
3.3.4 Muundo wa silabi usiofaa.....	45
3.4 Hitimisho	47

SURA YA NNE.....	49
4. 0 UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KISINTAKSIA	49
4.1 Utangulizi	49
4.2 Mifano ya makosa ya kisintaksia	51
4.2.1 Ukiushi wa viambishi vya nafsi.....	52
4.2.2 Matumizi mabaya ya vivumishi.....	53
4.2.3 Ukiushi wa kiambishi cha 'a' unganifu.....	55
4.2.4 Ukiushi wa viambishi vya hali ya udogo na ukubwa.....	56
4.2.5 Ukiushi wa viambishi vipatanishi vya ngeli.....	57
4.2.6 Matumizi mabaya ya vihusishi.....	58
4.2.7 Matumizi mabaya ya viunganishi.....	59
4.2.8 Matumizi mabaya ya virejeshi.....	60
4.2.9 Ukiushi wa viambishi vya mnnyambuliko wa vitenzi.....	61
4.2.10 Ukiushi wa viambishi vya njeo na hali.....	62
4.3 Hitimisho.....	63
SURA YA TANO	66
5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	66
5.1 Muhtasari	66
5.2 Hitimisho	67
5.3 Mapendekezo	68
MAREJELEO	71
VIAMBATISHO.....	74

ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

// Mabano ya fonimu

[] Mabano ya fonetiki

{ } Mabano ya mofu

\$ Mpaka wa silabi

K Konsonanti

I Irabu

Y Kiyeyusho

L1 Lugha ya kwanza

L2 Lugha ya pili

* Tungo isiyo sahihi

MAELEZO YA DHANA ZILIZOTUMIWA

Lugha ya kwanza (L1) - Hii ni lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza.

Pia hurejelewa kama lugha asilia au lugha ya mama.

Lugha ya pili (L2) - Ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha yake ya kwanza.

Lugha kadirifu - Ni lugha inayojitokeza wakati mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili.

Lugha hii huwa imekiuka kanuni za lugha lengwa hivi kwamba

hujitokeza kama lugha kamili yenyе mfumo wake wa kiisimu. Pia huitwa lugha kati.

- Makosa - Ni kanuni ambayo inakwenda kinyume na kanuni zilizowekwa. Isiyo sahihi.

Uchanganuzi Makosa - Ni mbinu itumiwayo kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha anayojifunza mwanafunzi. Mbinu hii huchunguza aina ya makosa na visababishi vya makosa hayo. Ni njia ya kupambanua, kuainisha na kufafanua makosa yanayofanywa na mtu anayejifunza lugha ya pili.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli wa mada

Lugha ya Kiswahili ina hadhi na majukumu mbalimbali nchini Kenya: Lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi inayotumiwa katika shughuli rasmi nchini Kenya. Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Kiswahili ni lugha ambayo inatumwiwa na watu ambao idadi yake yakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 60 ulimwenguni (Massamba 1999). Kiswahili ni lugha ya kimataifa na ni Lingua Franka inayotumiwa katika shughuli za biashara na mawasiliano katika Afrika Mashariki. Vyuo vingi ulimwenguni hufunza lugha ya Kiswahili. Vituo vya utangazaji hutangaza kwa lugha ya Kiswahili pamoja na lugha zingine. Kiswahili kimekuzwa sana nchini Kenya, kimefanywa kuwa somo la lazima katika shule za msingi na za upili katika mfumo wa 8 – 4 – 4.

Kwa kuzingatia hayo yaliyosemwa kuhusu lugha ya Kiswahili ni dhahiri kwamba lugha hii ni muhimu sana na ina mawanda mapana kimatumizi, tofauti na lugha zingine za Kibantu. Lugha hii imefanyiwa utafiti na uchunguzi mwengi na wataalamu mbalimbali wa lugha na historia. Lakini pamoja na umuhimu wake huo mkubwa, lugha hii imekumbwa na athari za lugha ya kwanza za wale wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Pana haja ya kutafiti na kutambua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayojitokeza katika kazi za wanafunzi ili tuweze kupendekeza njia ambazo walimu wanaweza kuwasaidia wanafunzi ili kuimarisha lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili na Ekegusii ni lugha za nasaba moja – Kibantu ambazo tunatarajia kufanana kwa kiasi fulani kimuundo na kiupatanisho. Pia zinatofautiana kwa kiwango

fulani. Lugha ya Ekegusii ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa magharibi mwa Kenya na watu wanaoitwa Wakisii. Wakisii wanapatikana katika mkoa wa Nyanza ambapo wanakaa katika kaunti mbili ; Nyamira na Kisii. Guthrie (1971) aliweza kuainisha lugha za kibantu katika makundi mbalimbali ambapo lugha ya Ekegusii aliiweka katika ukanda wa E kundi la 40, nambari ya E42.

Johnstone (1919), anasema kuwa lugha ya Ekegusii na Kiswahili ni lugha ambishi bainishi. Maana ya mzizi wa neno hubainika kwa kuongezewa viambishi awali na viambishi vifuutilizi. Viambishi hivi huwa na majukumu mbalimbali ya kisarufi.

Tutaangalia namna ambavyo aina mbalimbali za sentensi zimetumiwa na wanafunzi. Kwa vile sentensi hujengwa kwa maneno na nomino huainishwa katika ngeli tofautitofauti, ngeli na viambishi vyake huchukua nafasi kubwa kwa sababu baadhi ya maneno ya Kiswahili huambishwa ili kutupa habari za kisarufi hivyo basi kuleta uhusiano baina ya mofolojia na sintaksia.

1.2 Tatizo la utafiti

Kazi za wanafunzi zina makosa mbalimbali, makosa haya hutokana na athari ya lugha ya kwanza. Utafiti huu umejikita katika kuchunguza na kuchanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayojitokeza katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi. Makosa haya ni yale yanayodhahirika katika fonimu, muundo wa maneno, virai, vishazi na sentensi. Hata kama kumekuwepo na juhudzi za kuimarisha na kuiboresha lugha ya Kiswahili, utafiti unaonyesha kuwa wanafunzi wengi hufanya makosa katika mazungumzo yao na wanapoandika. Makosa haya huwa pingamizi katika kuimudu lugha ya Kiswahili.

Kutokana na kazi za wanafunzi zilizoandikwa, imedhihirika wazi kuwa makosa mbalimbali hujitokeza, hali ambayo inachangia matokeo duni kwenye somo la Kiswahili. Baadhi ya makosa hayo ni katika viwango vya mofolojia, fonolojia na sintaksia. Makosa haya yameibua hisia ya kuyashughulikia. Makosa katika viwango vingine yameshughulikiwa lakini hapana utafiti wowote ulioshughulikia makosa katika viwango hivi vitatu kwa pamoja hasa katika kazi za wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Ekegusii na wanajifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili.

Tafiti zilizofanywa zimeegemea zaidi katika lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili. Kwa mfano, Mwaniki (1999) alichunguza makosa ya kisintaksia yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha yao ya pili na lugha yao ya kwanza ni Kikuyu. Katika upande wa Kiswahili tafiti zimewahi kufanywa kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili, zimejikita zaidi katika matatizo ya kijumla, nyingi ni katika kiwango cha kimofolojia, kifonolojia na kimofosintaksia. Kwa mfano, Rapando (2005) alichunguza makosa ya kimofo-sintaksia yanayofanywa na wanafunzi katika shule za upili jijini Nairobi. Mutugu (2001) alichunguza na kuainisha makosa ya kileksia yanayojitokeza katika lugha za wanafunzi wa kidato cha pili. Naye Mbula (2011) alichunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kikamba wanapojifunza Kiswahili sanifu.

Tukiangalia tafiti hizi, hapana utafiti wowote uliorejelea makosa katika viwango hivi vitatu kwa pamoja yaani kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili hasa lugha yao ya kwanza ikiwa ni Ekegusii. Utafiti mmoja tu unaokaribiana na wetu na ambao umekuwa mchango mkubwa kwa kazi yetu ni wa Rapando (2005) ambaye alichunguza makosa ya kimofosintaksia lakini watafitiwa ni wazawa wa lugha tofauti. Mathalani, mwanafunzi

anayezungumza lugha ya Kikuyu huathirika tofauti na yule anayezungumza lugha ya Ekegusii. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa tunarejelea wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii na pia tunashughulikia viwango vitatu. Kutokana na tafiti zilizofanywa, matatizo yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza huhitilafiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

Hivyo tatizo letu linahusu makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayojitokeza katika kazi za insha zilizoandikwa na wanafunzi walio katika viwango viwili tofauti vya usomi. Wanafunzi tulio wahusisha ni wa kidato cha kwanza na tatu. Tulichagua vidato hivi kwa sababu katika kidato cha kwanza bado umilisi wa wanafunzi haujakomaa na katika kidato cha tatu umilisi wa wanafunzi umefikia ukomavu. Makosa haya ni kama vile: yale ya kudondo au kupachika sauti zisizopatikana katika Ekegusii, makosa mengine yalidhihirika katika miundo ya maneno isiyo sahihi. Aidha makosa mengine hutokea wakati mwanafunzi anahamisha mazoea ya lugha ya kwanza kwenda lugha ya Kiswahili. Makosa hutokea wakati sauti iliyo katika lugha ya Kiswahili haipatikani katika lugha ya Ekegusii.

Kutokana na maelezo tuliyotoa hapo juu, ni wazi kuwa kuna athari za lugha ya Ekegusii katika matumizi ya Kiswahili. Athari hizi huenda ndizo zinazosababisha makosa haya. Kama tulivyotaja hapo awali kuwa lugha hizi mbili ni za nasaba moja, tunatarajia kufanana kwa lugha hizi lakini ukweli ni kuwa, kwa kiwango fulani zinatofautiana. Kutokana na tofauti hizi mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili na lugha yake ya kwanza ni Ekegusii huathirika pakubwa sana. Corder (1981), anaeleza kuwa kila lugha ina muundo wake na kuhamisha sauti au mpangilio wa L1 katika L2 hudhihirika kama makosa. Hali hii ndiyo ilitupa msukumo wa kuyachunguza makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika matumizi ya Kiswahili Sanifu.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unanuia kutekeleza madhumuni yafuatayo:

1. Kuchanganua makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii .
2. Kuchanganua makosa ya kisintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii.
3. Kuchunguza tofauti za miundo ya silabi katika Ekegusii na Kiswahili Sanifu.
4. Kuchunguza ikiwa nadharia ya Uchanganuzi Makosa inafaa katika kuchanganulia makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii.

1.4 Nadharia tete

Utafiti umeelekezwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Kazi zilizoandikwa na wanafunzi wanaozungumza Ekegusii huwa na makosa ya kifonolojia na kimofolojia.
2. Kazi zilizoandikwa na wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii huwa na makosa ya kisintaksia.
3. Tofauti kati ya miundo ya silabi katika Ekegusii na Kiswahili sanifu huathiri matumizi ya Kiswahili.
4. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inafaa katika kuchanganulia makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada Hii

Pana haja ya kushughulikia makosa ya kifonolojia,kimofolojia na kisintaksia yanayotokana na athari za LI katika L2 kwa kuwa uchunguzi wa athari hizo utasaidia katika harakati za kujaribu kuyarekebisha makosa haya mionganoni mwa wanafunzi. Matokeo ya uchunguzi huu yatakuwa ya manufaa kwa walimu ambao wataweza kuyarejelea ili kutabiri uwezekano wa kutokea kwa makosa hayo katika matumizi ya Kiswahili Sanifu mionganoni mwa wanafunzi wanaozungumza Ekegusii.

Kwa hivyo, wataweza kuzishughulikia athari kama hizo kwa njia mwafaka.

Aidha Kiswahili ni lugha iliyo na majukumu mengi kama tulivyoeleza awali. Zaidi ya kuwa ni lugha inayotumiwa katika mawanda mapana kama vile siasa, utawala na biashara mionganoni mwa mengine, pia ni lugha inayowaunganisha wanajamii mbalimbali kwa kuwa hutumiwa na wazungumzaji ambao lugha zao za kwanza ni tofauti. Pia Kiswahili ni mojawapo kati ya masomo ambayo hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa. Utafiti huu utakuwa na mchango katika kusisitiza nafasi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa.

Kumekuwepo na tetesi kuwa wanafunzi hawafanyi vyema katika somo hili. Tetesi hizi ni za ukweli hasa tunapoangalia matokeo ya kitaifa ambayo hayaridhishi. Wanafunzi hupata matokeo duni sana katika somo hili. Matokeo haya yasiyordhisha ndiyo yaliyotupelekea kufanya utafiti ili kubainisha ni matatizo yepi wanafunzi hupata katika somo hili yanayochangia matokeo haya duni. Katika somo la lugha ikiwa mwanafunzi hatazingatia kanuni za lugha husika atafanya makosa hapa na pale

na makosa haya ndiyo pingamizi kubwa katika kuimudu lugha. Hata kama kumekuwepo na tetesi hizi hakuna tafiti za kutosha zimefanywa ili kutatua tatizo hili.

Utafiti huu utakuwa wa mchango kwa walimu wanaofunza somo la Kiswahili katika kaunti za Nyamira na Kisii. Walimu wataelewa matatizo yanayowakumba wanafunzi na kubuni mbinu za kutatua matatizo hayo. Pia, utafiti huu unaweza kuwafaa wanafunzi wa somo la Kiswahili.

1.6 Upeo na mipaka

Utafiti wetu umejikita katika kuchunguza makosa ya kifonolojia, kisintaksia na kimofolojia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wanaozungumza lugha ya Ekegusii na haujashughulikia lugha zingine. Athari za L1 kwa L2 zinatokea katika viwango vyote vya lugha yaani fonolojia, mofolojia na sintaksia. Utafiti huu umeshughulikia viwango hivyo vya lugha. Kwa sababu tumetaka kupata upatanisho wa kisarufi kwa kina, tumejikita katika makundi ya nomino(ngeli) na upatanisho wao. Pia tumeshughulikia mofu za njeo na upatanisho wa vipashio vyake. Isitoshe tumeshughulikia miundo ya silabi ya maneno katika lugha hizi. Kwa kiasi kikubwa tumeshughulikia fonimu, maneno, sentensi, virai na vishazi. Tumejiepusha na masuala yaliyoibuka kutokana na makosa mengine yaliyojitokeza na ambayo hayakuhusu tatizo la utafiti. Makosa haya ni ya msamiati, mtindo, uakifishaji n.k. Hii ni kwa sababu upeo wa tatizo la utafiti huu halijihusishi na makosa mengine yanayotokana na kategoria nzingine.

1.7 Msingi wa Kinadharia

Kuna mitazamo mbalimbali inayotumika kueleza jinsi mtu anavyojifunza lugha ya pili. Mitazamo hii ni kama vile Uchanganuzi Linganuzi, Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu. Katika utafiti huu tutaongozwa na mtazamo wa Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu. Kwa vile utafiti huu unanuia kuchanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya pili, mtazamo wa lugha kadirifu utaafiki tatizo hili la utafiti. Selinker (1969), anasema kuwa Lugha Kadirifu ni lugha inayoundwa na wanaojifunza lugha ya pili katika harakati zao za kuimudu lugha lengwa. Lugha Kadirifu hutofautiana na lugha ya kwanza ya mwanafunzi na lugha lengwa.

Uchanganuzi Makosa ni muhimu kwa sababu humwezesha mtafiti kujua jinsi watu hujifunza lugha na mikakati wanayotumia katika harakati za kutambua lugha lengwa (Corder, 1967:167). Wanaojifunza lugha hukiuka kaida za lugha ya pili. Uchanganuzi Makosa unatofautiana na Uchanganuzi Linganuzi kwa sababu hutilia maanani makosa yote yanayosababishwa na mambo mengine mbali na athari za lugha ya kwanza. Mihimili ya uchanganuzi makosa inapatikana katika Lugha Kadirifu.

1.7.1 Lugha Kadirifu

Lugha hii huwa imekiuka kanuni za lugha lengwa hivi kwamba hujitokeza kama lugha kamili yenyе mfumo wake wa kiisimu. Kwa mujibu wa Gas na Selinker (2008:14) inawezekana kuchanganua vipengele vingi vya lugha kwa kutumia mtazamo wa lugha kadirifu k.v. sarufi, fonolojia, mofolojia, sintaksia msamiati, pragmatiki na semantiki.

Selinker (1972) alibainisha mifanyiko ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika uchanganuzi wa Lugha Kadirifu. Mifanyiko hii ni kama ifuatayo:

1. Uhamishaji lugha ambapo kanuni na mifumo ya Lugha Kadirifu yaweza kutokana na L1. Wanafunzi hutumia lugha yao ya mama ili kuunda mifumo ya lugha legwa. Kwa kufanya hivi, sio kosa bali ni njia ambayo wanafunzi wengi hutumia kuunda mifumo ya lugha. Tofauti iliyopo baina ya kujifunza lugha ya kwanza na ya pili ni kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili huathirika na lugha ambayo tayari mwanafunzi anaijua. Kuathirika huku ndiko kunaitwa uhamishaji wa lugha. Uhamishaji lugha waweza kutokana na lugha ya kwanza, pili au tatu na hutokea katika viwango tofauti k.v. sarufi, matamshi, msamiati, diskosi, n.k.
2. Mikakati ya ufundishaji mbaya wa lugha ya pili kutokana na uelewa mbaya wa mwalimu, wa umilisi wa kiisumu pamoja na mbinu mbalimbali za ufundishaji wa lugha ya pili. Mwanafunzi hujifunza lugha kwa kusikia mwalimu wake anavyozungumza. Mwanafunzi anaposikia matamshi mabaya kutoka kwa mwalimu, naye hufanya makosa hayo bila kujua. Hii ni kwa sababu mwalimu ni mzungumzaji wa lugha ya kwanza na kwa hivyo katika kufundisha yeye hufanya makosa.
3. Ujumlishaji mno - Kanuni za lugha lengwa hujumlishwa. Wanafunzi hutumia kanuni za lugha ya pili namna ambavyo wazawa wa lugha hii hawawezi kutumia. Watafiti huamini kuwa miundo hii ya lugha hutokana na ujuzi alionao mwanafunzi katika akili yake. Mwanafunzi hujumuisha sifa za lugha pale ambapo sifa za lugha anayojua zinakaribiana na zile za lugha anayojifunza. Hii husababisha ucheleweshaji wa uelewa wa sifa tofauti.

Mwanafunzi anaweza kukataa kujifunza kanuni zilizo tofauti na lugha yake ya kwanza.

4. Mikakati ya kujifunza L2. Wanafunzi husahilisha sarufi ya L2 ili kufikia uamilifu mpana wa mawasiliano. Mwanafunzi anapojifunza lugha hutaka kurahisisha matamshi katika mawasiliano.
5. Mkakati wa kuwasiliana katika L2. Mawasiliano katika L2 hutokana na njia mahususi ambazo watu hujifunza ili kuweza kuwasiliana ili kukabiliana na upungufu wa L2.

1.7.2 Uchanganuzi Makosa

Mtazamo wa Uchanganuzi Makosa uliasisiwa na Corder na wenzake miaka ya 1960. Mtazamo huu uliibuka kukidhi upungufu wa uchanganuzi linganuzi uliotumiwa na wanaisimu kutofautisha lugha ya kwanza na ya pili ya mwanafunzi ili kukisia makosa. Uchanganuzi makosa ni mbinu itumiwayo kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha ya mwanafunzi. Walimu wa lugha wanaowasikiliza wanafunzi wao wakizungumza hutambua makosa. Ukweli ni kuwa kila mtu hufanya makosa anapoongea hata walimu na wazawa wa lugha hufanya makosa. Wazawa wa lugha hawafuati kanuni za sarufi zilizoandikwa vitabuni.

Uchanganuzi makosa, huchunguza aina ya makosa na visababishi vyta ya makosa hayo. Kulingana na wanaisimu Corder, mtafiti hufuata hatua zifuatazo katika uchanganuzi makosa:

1. Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha

2. Kutambua makosa
3. Kueleza makosa. Makosa yanawekwa katika makundi na kuelezwa kisarufi. Hivyo makosa yenye ndiyo hutumiwa katika kuainisha kategoria za kisarufi.
4. Kufafanua chanzo cha makosa haya.
5. Kutathmini / kuyasahihisha makosa haya ili kujua jinsi ya kukabiliana nayo.

Tunapowasikiza wanafunzi wakizungumza tunafahamu makosa wayafanyayo. Kwa sababu hii ni vyema kujiuliza kile mzungumzaji alikusudia kukisema na angekisema vipi. Kusahihisha makosa haya sio jambo rahisi kwa sababu kuna zaidi ya njia moja ya kufanya hivyo. Kusahihisha makosa kunategemea kile msikilizaji anafikiri mzungumzaji alikusudia kukisema na kosa lenyewe. Ni vyema kufikiri namna nyingi tofauti za kusahihisha makosa. Kwa sababu huna uhakika wa kilichokusudiwa, mwache mwanafunzi akusaidie kuamua sahihisho sahihi.

Kufafanua makosa haya, kwataka kujua kisababishi. Makosa yanaweza kutokana na kuhamisha kanuni au ruwaza za lugha ya kwanza. Makosa mengine yanaweza kusababishwa na jinsi mwalimu au vitabu vya kaida vinavyoeleza kanuni fulani. Au inaweza kuwa mikakati ya mawasiliano anayotumia mwanafunzi hata kama anajua kanuni anazotumia sio sahihi.

Utafiti huu si linganishi kwa sababu hatujalinganisha lugha mbili ili kutambua makosa. Kwa hivyo Mtazamo wa Uchanganuzi Linganishi hautafaa katika utafiti wetu. Aidha, utendaji wa wanafunzi katika uandishi wa insha hauwezi kuchunguzwa kwa kutumia mtazamo huu. Katika utafiti huu tumetumia mitazamo miwili nayo ni Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu kwa kuwa ndiyo hutilia maanani makosa yote yanayosababishwa na mambo mengine mbali na athari za L1.

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu somo hili

1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu lugha ya Kiswahili na Ekegusii

Polome (1967), ametoa maelezo kuhusu sarufi ya Kiswahili. Maelezo haya ni kuhusu virai, vishazi na viambishi nya njeo, vipatanishi na ukanushaji pamoja na ngeli nomino zake. Maelezo haya yatakuwa na manufaa kwetu sana katika kulinganisha baadhi ya mambo ya kimofolojia, kisintaksia na kifonolojia ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii.

Kihore na wengine (2001), wametoa maelezo kuhusu kategoria mbalimbali za maneno, viambishi nya vitenzi vikiwemo nya njeo, vipatanishi nya nafsi na yambwa. Maelezo haya yatatusaidia katika kuelewa kategoria za kisarufi.

Rapando (2005), alichunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi. Katika utafiti wake, Rapando aligundua kwamba baadhi ya makosa yanababishwa na lugha ya kwanza, Kiingereza na Sheng. Aidha, ujumlishaji mno ulidhihirika kusababisha makosa ya kimofosintaksia. Utafiti wetu ni tofauti kwani umelenga kundi mahususi.

Otiende (2013), alichunguza athari za kimofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Utafiti huu ulidhihirisha kuwepo kwa tofauti kubwa baina ya mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kiolusuba ambayo huathiri matumizi ya Kiswahili. Aidha utafiti huu umelinganisha miundo ya silabi za Kiolusuba na za Kiswahili ambapo amepata ni tofauti. Tofauti hii amepata inachangia katika athari hiyo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani haukushughulikia kiwango cha kisintaksia na hivyo hakujishughulisha na miundo ya sentensi na upatanisho wa kisarufi.

Guthrie (1948), alijishughulisha na lugha za Kibantu kwa ujumla. Aliziweka lugha hizi katika makundi. Kazi yake itatusaidia kujua lugha ya Ekegusii na Kiswahili ziko katika kundi gani.

Osinde (1988), alishughulikia mabadiliko ya kimofolojia ya konsonanti za Ekegusii. Katika sura ya 3, alichunguza kipengele cha mofolojia ya nomino na kitenzi. Sehemu hii itakuwa ya manufaa kwetu kwani nomino na kitenzi ndio hujenga sentensi.

Gesare (1992), alijishughulisha na mofolojia ya lugha ya Ekegusii kwa kutumia nadharia ya umuundo. Kazi yake itatufaidi sana kwani itatusaidia kuelewa muundo wa nomino na kitenzi katika lugha ya Ekegusii.

Mayaka (2000), alichunguza na kujadili muundo wa sentensi katika lugha ya Ekegusii akitumia nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo. Alitazama sentensi sahili, ambatani na changamano. Kazi hii yake itakuwa ya manufaa kwetu, kwani kazi za wanafunzi zimejengwa na sentensi mbalimbali. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu alijikita katika muundo wa sentensi ya Ekegusii na alitumia nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo. Katika utafiti wetu tunachanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi kwa kutumia mitazamo ya Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu.

Kimapokeo, sarufi iligawanywa katika vikundi viwili: mofolojia na sintaksia. Mofolojia hujihusisha na maumbo ya maneno ilhali sintaksia hujihusisha na uchanganuzi wa mpangilio na uhusiano wa upatanisho katika virai na sentensi (TUKI 1990). Maeleo haya yatatuzaa katika kuelewa maumbo ya maneno na uhusiano wa upatanisho uliopo baina sentensi mbalimbali.

Radford (1997: 6), anasema kuwa sarufi inapaswa kuwa sahili kama iwezekanavyo ili kuwe na utendaji kazi wa viambajengo vyta kisarufi. Viambajengo huwa ni sehemu ya mofolojia ya

kuunda maneno. Sehemu hii itatusaidia katika kuainisha makosa ya kimofolojia yanayojitokeza katika kazi za wanafunzi.

Maneno huwekwa katika kategoria za kisarufi. Kategoria ni kundi la maneno yaliyo na sifa zinazofanana ambazo hugawana seti za sifa za kisarufi. Mofolojia hujitokeza katika mofolojia ya unyambuaji na mofolojia ya uambishaji. Sifa ya uambishaji hujumulisha mofu za uambishaji ambazo hufungamanishwa na nomino na kitensi kuonyesha uamilifu mbalimbali wa kisarufi wa neno. Sifa za unyambuaji hujumulisha mofu za unyambuaji ambazo hutumiwa kuunda maneno ya kategoria tofauti kwa kutumia shina la neno (Yule 1996: 74-75). Sifa hizi zitatusaidia katika kuchanganua makosa yanayojitokeza katika kazi za wanafunzi.

1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Lugha Kadirifu na Uchanganuzi

Makosa.

Kulingana na Corder (1967), Uchanganuzi Makosa ni muhimu kwa sababu humwezesha mtafiti kujua jinsi watu hujifunza lugha na mikakati wanayotumia katika harakati za kutambua lugha lengwa. Wanaojifunza lugha hukiuka kaida za lugha ya pili. Wanafunzi wa lugha ya pili mara nyingi huhamisha usemi wa lugha ya kwanza na kutumia sheria zake katika lugha ya pili.

Corder (1967), anaeleza kuwa matatizo yanayojitokeza mtu anapojifunza lugha ya pili ni jambo la kawaida kutokea. Kabla ya mwanafunzi kuzoea matumizi kamili ya kanuni za lugha ya pili hufanya makosa hapa na pale. Corder (1967) anatofautisha makosa na matatizo yanayotokea mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili. Kulingana naye, makosa ni matatizo yanayotokana na utendaji na hayana kikwazo chochote na yanaweza kutokea katika hali zozote. Hata hivyo makosa yanadhihirika kwa kuzingatia umilisi na utendaji wa lugha.

Selinker (1969), ameeleza mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Mifanyiko hiyo ni pamoja na: ujumlishaji mno kutokana na mifumo ya L1 inayotumiwa kiholela, uhamishaji wa kanuni za L1 hivyo kukiuka kanuni za L2, mikakati ya mawasiliano katika L2, njia za kujifunza zisizokuwa halisi na uhamishaji wa ufundishaji ambapo makosa hutokana na kutokuwa na umilisi kwa wanaofundisha. Kulingana naye, makosa haya yanaibua kiwango kingine katika matumizi ya lugha ambacho ni Lugha Kadirifu. Lugha Kadirifu ni lugha inayojitokeza wakati ambapo mzungumzaji yuko katika harakati za kujifunza lugha ya pili. Mzungumzaji wa lugha kadirifu huhamisha kanuni za lugha ya kwanza kwa lugha lengwa. Kazi hii ya Selinker itachangia katika kazi yetu kwa kuwa itatuwezesha kuyabainisha makosa kwa kutumia baadhi ya vigezo alivyovitaja. Kazi ya Selinker (1969) ilishughulikia lugha kwa ujumla kwetu tutashughulikia makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia kwa lugha mahususi Ekegusii kwa Kiswahili.

Selinker (1972), anaeleza kuwa mfumo huu mpya unaojitokeza unaweza kuchunguzwa kwa kushirikisha wanaojifunza lugha ya pili katika maandishi na mazungumzo. Aligundua kwamba kadri mwanafunzi anavyozidi kujifunza ndivyo matatizo yanavyozidi kudidimia. Kauli hii tunatazamia kuithibitisha katika utafiti wetu. Sampuli yetu itakuwa na wanafunzi wenye umilisi tofauti katika Kiswahili.

Kazi ya Selinker (1972), itatusaidia kuelewa mtazamo wa Lugha Kadirifu. Lugha Kadirifu ni lugha inayoundwa na wanaojifunza lugha ya pili katika harakati zao za kuimudu lugha lengwa. Lugha Kati hutofautiana na lugha ya kwanza ya mwanafunzi na lugha lengwa. Selinker anasisitiza kwamba, mfumo huu tofauti wa kiisimu unaweza kuchunguzwa kwa kushirikisha wanaojifunza lugha ya pili katika maandishi au mazungumzo. Anasema kuwa lugha kati hubadilikabadilika kulingana na muktadha.

Lugha Kadirifu huwa imekiuka kanuni za lugha lengwa hivi kwamba hujitokeza kama lugha kamili yenyeye mfumo wake wa kiisimu. Kwa mujibu wa Gas na Selinker (2008:14) kwa kutumia mtazamo wa Lugha Kadirifu tunaweza kuvichanganua vipengele vya lugha kama vile sarufi, fonolojia, mofolojia, msamiati, pragmatiki na semantiki.

1.9 Mbinu za Utafiti

Ili kufikia malengo ya utafiti kwa njia mwafaka katika mipaka ya nadharia husika harakati za utafiti lazima zishughulikiwe kwa utaratibu. Utafiti huu ni utafiti fafanuzi, kwani ni kazi inayochunguza data na kueleza jinsi ilivyo. Ekegusii ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa katika kaunti za Nyamira na Kisii.

1.9.1 Mbinu za kukusanya data

Tumetumia sampuli ya wanafunzi arobaini mionganini mwa wazungumzaji wa Ekegusii. Sampuli yetu tumeipata kutoka kwa shule ya upili ya Ekenyoro na Rirumi zinazopatikana katika kaunti ya Nyamira. Kuna shule nyingi katika kaunti hizi lakini tumechagua shule hizi kwa sababu zinapatikana katikati mwa eneo ambapo lugha ya Ekegusii huzungumzwa na watoto takribani wote. Watoto hawa hutumia lugha hii kama lugha ya kwanza nyumbani. Tumetumia data tulioipata kutoka kwa wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Wanafunzi tuliowahusisha ni wa kidato cha kwanza na cha tatu. Tulichagua vidato hivi kwa sababu katika kidato cha kwanza bado umilisi wa wanafunzi haujakomaa na katika kidato cha tatu umilisi wa wanafunzi umefikia ukomavu. Tumetumia sampuli ya wanafunzi arobaini; ishirini kutoka kila shule na kila kidato wanafunzi kumi. Kwa mfano, katika shule ya upili ya Ekenyoro ina wanafunzi hamsini katika kidato cha kwanza, ili kuwateua wanafunzi kumi kutoka kidato hiki, tuliwapa nambari moja hadi tano, bila kufuata utaratibu wowote tuliteua wanafunzi waliokuwa nambari ya nne. Wanafunzi hawa ndio tulioatumia kama sampuli

yetu. Tulifanya hivyo katika vidato vingine. Wanafunzi hao walipewa insha za kuandika ambazo tulizisahihisha kwa makini na kujaribu kuyachanganua makosa yao huku tukyaainisha katika makundi kulingana na aina zake.

1.9.2 Mbinu za kuchanganulia data

Baada ya kupata data kutoka nyanjani, makosa yaliainishwa baada ya insha za wanafunzi kusahihishwa ili kubaini makosa. Makosa yaliwekwa katika kategoria. Kila kosa liliwekwa kulingana na kategoria yake. Ikiwa kosa ni la kisarufi liliwekwa katika kategoria ya kisarufi lile la kifonolojia liliwekwa katika kategoria hiyo. Baada ya kuyaainisha makosa na kuyaweka katika kategoria tofauti. Tulitoa maumbo sahihi na kueleza visababishi vyta makosa hayo.

1.10 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa kama kirejelewa kwa watafiti wa baadaye. Utafiti huu utatoa mchango kwa wasomi wa Kiswahili kwani ni tafiti chache zimefanywa kuhusu uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia kwa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unaweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili wanaofunza katika kaunti za Kisii na Nyamira kuelewa matatizo yanayowakumba wanafunzi na kutafuta mbinu mwafaka kukabiliana na matatizo hayo. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika usomi wa kiisumu. Wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili wataelewa changamoto watakazokumbana nazo na jinsi ya kukabiliana nazo. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha sehemu ambazo wanafunzi wanahitaji msaada zaidi wanapojifunza Kiswahili Sanifu. Wakuza mitaala na walimu watayatambua makosa yanayowakabili wanafunzi wa lugha ya Kiswahili na kuona jinsi watakavyorekebisha hali hii.

SURA YA PILI

2.0 FONIMU NA SILABI ZA KISWAHILI SANIFU NA EKEGUSII

2.1. Utangulizi

Sura hii imeshughulikia fonimu za Kiswahili sanifu na za lugha ya Ekegusii. Ni muhimu kutoa ufanuzi wa uwanja wa fonolojia. Kwa mujibu wa (TUKI 1990:46) fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumiwa katika lugha fulani. Kiswahili na Ekegusii ni lugha asilia za Kibantu. Lugha hizi zina sifa za sauti za kimsingi zinazowiana. Hata hivyo lugha mbili asilia haziwezi kuwa sawa katika vipengele vyote vya sauti.

Kipengele cha uchanganuzi katika fonolojia ni fonimu. Fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha kifonolojia kinachobadili maana ya neno (TUKI 1990:45). Fonimu ni kitamkwa kilichobainifu katika lugha fulani maalumu (Massamba na wengine, 2004). Kwa mfano, fonimu /p/ na /b/ katika Kiswahili sanifu ni sauti bainifu. Katika Kiswahili sanifu maneno [paa] na [baa] yana fonimu sawa isipokuwa sauti za kwanza [p] na [b]. Fonimu hizi ndizo zinazotofautisha maana ya maneno haya. Sauti fulani ikiondolewa katika neno na kuwekwa sauti tofauti maana ya neno hilo itabadilika na sauti hizi ndizo fonimu. Iwapo sauti moja itakosa kuleta maana katika lugha fulani ,sauti hiyo itakosa hadhi yake kama fonimu.

Ili kuelewa lugha vizuri ni muhimu kuanzia kwenye kiwango cha sauti za hiyo lugha. Huwezi kuimudu lugha vizuri kama huelewii sauti zake. Tutaeleza fonimu za lugha hizi mbili katika sehemu hii.

2. 2 Fonimu za Kiswahili sanifu

Wanaisimu kama vile Polome (1967), Mgullu (1999), Massamba na wenzake (2004) na Iribemwangi (2010) wameziainisha fonimu za Kiswahili sanifu kama:

i. Fonimu za irabu.

ii. Fonimu za nusu irabu.

iii. Fonimu za konsonanti.

Kiswahili sanifu kina irabu tano nazo ni; /a/ , /ɔ/, /i/, /ə/ na /u/. Sauti hizi za irabu ndizo huungana na konsonanti ili kuunda silabi. Irabu hutamkwa pasipo kuzuiliwa hewa popote kinywani kinyume na konsonanti zinazotamkwa kwa kuzuiliwa hewa kinywani. Lugha ya Kiswahili sanifu ina nusu irabu mbili. Nusu irabu ni sauti zinazotamkwa kwa kuachilia hewa kutoka mapafuni kupitia kinywani au kwenye mkondo hewa wa pua kwa mkwaruzo mdogo. Fonimu hizi ni /w/ na /j/. Sauti hizi hudhihirika katika mifanyiko ya kifonolojia hasa katika uyeyushaji.

Wataalamu wengi wametofautiana kuhusu idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili sanifu. Polome (1967) ameordhesha konsonanti 24, Mgullu (1999) amesawiana na Polome, Massamba na wenzake (2004) wameainisha konsonanti 23, naye Iribemwangi (2010) ameordhesha konsonanti 25. Utafiti huu umeafikiana na Massamba na wenzake. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004:28), konsonanti ni sauti za lugha zinazotamkwa wakati ambapo hewa inayotoka mapafuni huzuiliwa kabisa au kidogo hivi kwamba nafasi ya hewa kupita ni ndogo sana hewa hupita na mkwaruzo. Konsonanti za Kiswahili sanifu ni /p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/, /c/, /ʃ/, /f/, /v/, /θ/, /ŋ/, /s/, /z/, /h/, /χ/, /m/, /n/, /ɲ/, /l/, /r/ na /r/.

Fonimu hizi zimeelezwa kimuhtasari katika jedwali lifuatalo:

Jinsi	Mahali pa kutamka	Midomo	Midomo-meno	Meno	Ufizi	Kaakaa-gumu	Kaakaa-laini	glota	Jumla
Kutamka									

Vipasuo	p, b			t, d	c, tʃ	k, g		8
Vikwamizwa		f, v	θ,	s, z	ʃ	γ	h	9
Nazali	m			n	ɲ			4
Kitambaza				l				1
Kimadende				r				1

Jedwali 1: Konsonanti za Kiswahili Sanifu

Mungania anatofautiana na wataalamu wengine kuhusu ishara ya fonimu /tʃ/, anapendekeza kuwa ishara ya fonimu hii inafaa kuwa /ç/. Aidha anadai kuwa fonimu /ç/ na /ʃ/ sio vizuiwakwamizwa bali ni vipasuo, “mazungumzo ya kibinagsi.” Katika utafiti huu tumetumia ishara hii.


2.3 Fonimu za Ekegusii

Katika lugha nyingi, fonimu zimegawika katika makundi mawili nayo ni: konsonanti na irabu. Fonimu huweza kutamkwa kwa kuachilia mkondo wa hewa mpana au kwa kuzuiliwa.

2.3.1 Fonimu za irabu za Ekegusii

Ekegusii kina irabu saba, nazo ni /a/, /e/, /ɪ/, /i/, /o/, /ɔ/ na /u/. Kwa mujibu wa Nyakundi (2010: 10) , Ekegusii kina irabu tano, nazo ni: /a/, /e/, /i/, /o/ na /u/. Irabu /e/ inajulikana kama irabu ya kati kama vile katika maneno kama /egete/ (kijiti) na /ekerito/ (kizito), lakini

irabu /◻/ ni irabu wazi kama vile katika maneno /ejaje/ (yako). Irabu (◻) ni nusu wazi kama vile katika maneno /r◻ra/ (kuona) na /r◻sa/ (kuchoka) lakini irabu /o/ ni ya kati kama vile katika /oβokima/ (ugali) na /soka/ (kuona haya). Katika utafiti huu tutachukua msimamo huu wa irabu saba. Irabu zimeainishwa kwa kutumia mchoro ufuatao:



Kutokana na maelezo ya hapo juu, ni wazi kuwa kuna homografu - neno lenye tahajia sawa na lingine lakini maana au matamshi ni tofauti. Kama inavyodhishirika katika mifano ifuatayo:

- 1 (i) (a) / \square s \square s \square / (mambo yameenda mrama)
 (b) /esese/ (mbwa)

 (ii) (a) /s \square ka/ (valisha)
 (b) /soka/ (haya/soni)

 (iii) (a) /enda/ (tumbo)
 (b) / \square nda/ (chawa/funza)

Matumizi ya irabu /*o*/, /*e*/, /*ø*/ na /*o*/ hutuwezesha kutofautisha maana ya maneno yaliyo na tahajia sawa lakini maana ya maneno hayo ni tofauti.

2.3.2 Konsonanti za Ekegusii

Lugha ya Ekegusii ina konsonanti 20 nazo ni: /t/, /d/, /k/, /g/, /C/, /nC/, /m/, /n/, /ŋ/, /l/, /w/, /j/, /β/, /s/, /ns/, /mb/, /nt/, /nd/, /g/ na /k/. Kwa mujibu wa Komenda (2011:28), Ekegusii kina konsonanti 22. Komenda alijumuisha sauti /mm/ na /nn/ kama konsonanti lakini hizi ni sauti zisizo na maana zinazotumiwa katika mazungumzo kama vile aaaa, eeee lakini hazitumiki katika maneno ya Ekegusii. Katika utafiti wetu hatutajumuisha sauti hizo. Kwa hivyo tutatumia konsonanti 20. Konsonanti hizi zimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo. Jedwali hili linaonyesha aina na mahali pa kutamkia konsonanti hizo

Mahali pa kutamkia Jinsi ya kutamka	Mdomo	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini
Vipasuo		t		k, g,
Vizuiwa-kwamizwa			C, nC	
Nazali	m	n	ŋ	
Nusu irabu	w		j	

Vikwamizwa	β	s,ns		
Kimadende		r		
Nazali-Ambatani	mb	nt, nd		k, g

Jedwali la 2. Jedwali la konsonanti za Ekegusii.

Konsonanti hizi huwasilishwa kama ifuatayo kifonetiki,

Fonimu	Othografia	Mifano	Fasiri
/β/	b	baba	mama
/mb/	mb	embura	mvua
/m/	m	amaino	meno
/t/	t	tata	baba
/nt/	nt	omonto	mtu
/nd/	nd	enda	tumbo

/n/	n	buna	vunja
/r/	r	rara	lala
/s/	s	soka	valisha
/č/	ch	amache	maji
/nč/	nch	inchwo	kuja
/ɲ/	ny	enyong'ora	jongoo
/j/	y	yaya	hapana
/k/	k	okogoro	mguu
/g/	g	igoro	juu
/ ̄ /	ng'	eng'ombe	ng'ombe
/ k/	nk	enka	mji
/ g/	ng	engabi	swara
/w/	w	kweba	sahau
/ns/	ns	ense	dunia

Tunapochunguza fonolojia ya Ekebusii na Kiswahili tunagundua tofauti iliyopo. Katika lugha ya Ekebusii konsonanti zifuatazo hazipo katika othografia ya lugha hii: b, p, d, ʃ, f, v, h, l,

ʃ, , ڏ, χ na z lakini katika lugha ya Kiswahili konsonanti hizi hutumiwa. Pia katika irabu , lugha ya Kiswahili ina irabu tano ilhali lugha ya Ekegusii ina irabu saba. Katika sura hii tumeshughulikia fonimu za Kiswahili sanifu na za Ekegusii. Aidha, tumbainisha fonimu zinazopatikana katika kila mojawapo ya lugha hizi ambazo zinatofautisha mifumo yake ya kifonimu.

Lugha ya Ekegusii inapoingiliana na lugha ya Kiswahili, matokeo huwa kukiuka kanuni za kisarufi na sauti za Kiswahili hutamkwa au kuandikwa vibaya na mpangilio wa maneno huvurugika na hili hutatiza mawasiliano. Makosa haya hutokea wakati mwanafunzi anahamisha mazoea ya lugha ya kwanza kwenda lugha ya Kiswahili. Makosa haya hutokea katika ngazi mbalimbali. Kama vile katika ngazi ya sauti, makosa hutokea wakati sauti aliyozoea mwanafunzi katika lugha yake ya Ekegusii haipatikani katika lugha ya Kiswahili. Hivyo hutumia sauti iliyo karibu nayo. Kwa mfano:

2. (i) papa badala ya baba
(ii) samani badala ya thamani
(iii) rara badala ya lala

Kuna hali ambapo watu huchanganya matumizi ya sauti kwa sababu ya kuathirika na lugha ya kwanza. Kwa mfano:

3. (i) chioni badala ya jioni
(ii) tawa badala ya dawa
(iii) mkumba badala ya mgumba

Athari nyingine inayowakumba wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii ni kudondoa au kupachika fonimu /h/ mahali isipohitajika. Fonimu hii haipatikani katika lugha ya Ekegusii kwa sababu hii wanafunzi hutumia fonimu hii visivyo. Kwa mfano:

4. (i) hama badala ya ama

(ii) ana badala ya hana

(iii) huna badala ya una

Makosa mengi sana hudhihirika wakati wanafunzi wanakanusha sentensi. Wanafunzi husahahu kiambishi kikanushi /h/. Kwa mfano mwanafunzi anakanusha sentensi “ Mtoto anacheza.” kama “Mtotoachezi.” Badala ya “Mtoto hachezi.”

Baadhi ya wanafunzi hupuuza mofu za Kiswahili na kuuongeza zile zinazopatikana katika lugha ya kwanza au huongeza mofu kwenye neno. Kwa mfano:

5. (i) naendaga badala ya naenda

(ii) anasomanga badala husoma

(iii) wanakulanga badala hula

Kutokana na mifano hapo juu ni dhahiri kuwa lugha ya Ekegusii huathiri pakubwa sana lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hutatizwa na lugha ya Kiswahili kwa sababu fonimu walizozoea katika lugha ya kwanza hazipatikani katika lugha ya Kiswahili au zile zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili hazipatikani katika lugha ya Ekegusii. Makosa haya yote hutokea kwa sababu ya tofauti iliyopo ya kifonimu baina ya lugha hizi mbili.

2.4 SILABI ZA KISWAHILI SANIFU NA EKEGUSII

Katika sehemu hii tutajadili tofauti za kumuundo za silabi za Kiswahili na Ekegusii. Tofauti hizi zitajikita katika kiwango cha fonolojia. Matatizo mengi yanayowakumba wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii wanapo jifunza lugha ya Kiswahili hutokana na tofauti za kumuundo zilizopo kati ya lugha hizi mbili. Hata hivyo twajua lugha hizi ni za kibantu kwa hivyo kuna uwezekano wa kufanana kumuundo kwa pakubwa.

Kulingana na Crystal (1991), silabi ni kipashio cha kifonolojia kilicho kikubwa kuliko fonimu lakini kidogo kuliko neno. Kipashio hiki hueleza muundo wa kifonolojia wa neno au maneno. Silabi huweza kuwa sauti moja tu, sauti mbili au zaidi. Massamba na wenzake (2004), wanaeleza kuwa kila silabi huwa na irabu kama kilele chake. Lugha nyingi za kibantu haziruhusu maneno kuishia kwa silabi fungo.

Kuna aina mbili za silabi: silabi huru na silabi fungo. Silabi huru huishia na irabu, silabi fungo ni zile ambazo huishia na konsonanti. Katika muundo wa silabi za lugha ya Kiswahili kuna miundo ya silabi iliyotokana na lugha za kigeni na inadhihirika katika maneno ya mkopo kama vile: bustani, tanbihi, daktari, alfabeti, n.k. Aidha kuna miundo ya silabi asili ya lugha ya Kiswahili.

2.4.1 Muundo wa Silabi katika Kiswahili sanifu

Kwa mujibu wa Iribemwangi (2008:70), Kiswahili kina miundo tisa ya silabi. Katamba (1992), ameeleza kuwa muundo wa silabi ndio hutupa kanuni ambazo zinatawala matumizi ya lugha fulani. Miundo ya silabi ya Kiswahili ni kama ifuatayo;

2.4.1.1 Muundo wa silabi pendwa (KI)

Muundo huu ndio msingi wa miundo yote ya silabi. Huu ndio muundo ambao hutumika takribani na lugha zote ulimwenguni. Muundo huu huitwa muundo wa silabi pendwa; lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kibantu hupendelea muundo ambapo konsonanti hufuatwa na irabu na neno kuishia kwa irabu. Sifa hii hufanya maneno yaliyokopwa kutoholewa ili yakubaliane na muundo wa lugha pokezi . Kwa mfano neno la Kiarabu “waqt” linapokopwa katika Kiswahili huwa “wakati”. Mfano wa maneno yenye muundo huu ni;

6. (a) /ma \$ ma/ (KI\$KI)
(b) /ki \$ ta \$ bu/ (KI\$KI\$KI)

2.4.1.2 Muundo wa konsonati konsonati irabu(KKI)

Muundo huu huhusisha mojawapo kati ya nazali tano katika nafasi ya kwanza. Kisha inafuatwa na kikwamizwa au kipasuo, nafasi ya mwisho huchukuliwa na irabu.kwa mfano,

7. (a) /mbu \$ zi/ (KKI\$KI)
(b) /nd \square \$ g \square / (KKI\$KI)

2.4.1.3 Muundo wa konsonanti kiyeyusho irabu (KYI)

Katika muundo huu, konsonanti huchukua nafasi ya kwanza, ikafuatwa na kiyeyusho kisha irabu inachukua nafasi ya mwisho.Kuna maneno yaliyo na muundo huu kwa mfano;

8. (a) /mw \square \$ w \square / (KYI \$ YI)
(b) /pwe \$ za / (KYI \$KI)

2.4.1.4 Muundo wa konsonanti, konsonanti, kiyeyusho na irabu (KKYI)

Muundo huu huwa na konsonanti ya nazali mwanzoni, kisha ikafuatwa na konsonanti hasa kipasuo, kisha kiyeyusho ambacho hufuatwa na irabu. Katika lugha ya Kiswahili sio maneno mengi yaliyo na muundo huu. Mifano wa baadhi ya maneno ni;

9. (a) /mbwe \$ ha / (KKYI \$ KI)
(b) /u \$g \square \$ n \ddot{u} wa/ (I \$ KI\$ KKYI)

(c) /ja\$ngwa/ (KI\$KKYI)

2.4.1.5 Muundo wa irabu pekee (I)

Muundo huu huwa na irabu pekee inayojisimamia kama silabi. Mara nyingi irabu hizo hufuatana pekee bila kuungana na konsonanti. Mifano ya maneno yenye muundo huu:

10. (a) /ta \$ a/ (KI\$ I)
(b) /ɔ\$a/ (I\$I)

2.4.1.6 Muundo wa konsonanti pekee (K)

Katika muundo huu, nazali hutumika lakini si nazali zote. Nazali /m/ na /n/ ndizo hutumika. Nazali hizi hutokea kama silabi mwanzoni na katikati mwa neno lakini sio mwishoni. Mifano;

11. (a) /m\$t□\$t□/ (K\$KI\$KI)
(b) /m\$cwa/ (K\$KYI)

2.4.1.7 Muundo wa konsonanti irabu irabu (KII)

Muundo huu hutokea pale ambapo konsonanti hufuatwa na irabu mbili. Mfuatano huu wa irabu huwa irabu ndefu. Nafasi ya kwanza huchukuliwa na konsonanti kisha kufuatwa na irabu mbili za aina moja. Hata hivyo katika Kiswahili sanifu muundo huu hautumiki sana.

Kwa mfano:

12. (a) /daawa/ /da:wa/ (KII \$ KI)
(b) /miiko/ /mi :ko/ (KII\$KI)

2.4.1.8 Silabi fungo

Silabi za aina hii huwa na konsonanti mwishoni mwa silabi. Silabi huonekana imefungwa na konsonanti iliyokaa mwishoni mwa silabi hiyo. Muundo huu hautumiki sana katika Kiswahili. Maneno mengi yaliyo na muundo huu ni yaliyokopwa kutoka kwa lugha zisizo za kibantu mifano ya maneno yaliyo na muundo huu;

13. (a) /ham\$ si \$ ni/ (KIK\$KI\$KI)
(b) /dak \$ ta \$ ri/ (KIK\$KI\$KI)

Hata hivyo ni mawazo yanayopingwa na Massamba na wenzake (2004), kwamba Kiswahili sanifu hakina muundo huu.

2.4.1.9 Muundo wa konsonanti konsonanti konsonanti irabu (KKKI)

Muundo huu huwa na konsonanti tatu zinazofuatana na mwisho huwa na irabu. Pia muundo huu hudhihirika tu katika maneno yaliyokopwa kama muundo wa silabi fungo, maneno haya yametoholewa kutoka lugha zingine hasa za kigeni. Mifano ya maneno katika muundo huu ni:

14. (a) /skru \$ bu/ (KKKI \$KI).
(b) /spri\$ngi/ (KKKI\$ KKI)

2.4.2 Muundo wa silabi katika lugha ya Ekegusii

Hata ingawa lugha ya Ekegusii na Kiswahili ni za Kibantu kama tulivyotaja hapo awali, lugha hizi zina tofauti zake, hata ingawa zinakaribiana kufanana kimuundo, Ekegusii kina muundo wa silabi wa konsonanti ikifuatwa na irabu. Miundo ya silabi katika Ekegusii ni kama ifuatayo;

2.4.2.1 Muundo wa konsonanti na irabu (KI)

Lugha za Kibantu hupendelea muundo wa silabi wenye mfuatano wa konsonanti na irabu. Muundo huu ni wa silabi pendwa. Mifano ya maneno katika lugha ya Ekegusii yenye muundo huu ni,

15.	Ekegusii	Fasiri
(a)	/□\$m□\$t□/	mti
(b)	/□\$ka\$ra\$mu/	kalamu
(c)	/□\$g□\$ta\$bu/	kitabu

2.4.2.2 Muundo wa konsonanti konsonanti irabu (KKI)

Konsonanti za nazali huchukua nafasi ya kwanza zikifuatwa na konsonanti za vipasuo na nafasi ya mwisho huchukuliwa na irabu yoyote. Mifano ya maneno yenye muundo huu ni:

16.	Ekegusii	Fasiri
------------	-----------------	---------------

- | | |
|-------------------|--------|
| (a) /□\$m□\$ nt□/ | mtu |
| (b) /□\$ŋ□\$mba/ | nyumba |
| (c) /ći& □\$ni/ | mboga |

2.4.2.3 Muundo wa konsonanti kiyeyusho irabu (KYI)

Katika muundo huu konsonanti huchukua nafasi ya kwanza, zikafuatwa na kiyeyusho hatimaye nafsi ya mwisho huchukuliwa na irabu.

Mifano ya maneno yenye muundo huu ni:

17. Ekegusii	Fasiri
(a) /□\$mwa\$ ka/	mwaka
(b) /□\$b□\$rwa \$i\$r□/	ugonjwa
(b) /gw□ \$ na /	pona

2.4.2.4 Muundo wa irabu pekee (I)

Muundo huu uko katika lugha ya Ekegusii na hujitokeza katika maneno mengi kinyume na ilivyo katika Kiswahili. Hii ni kwa sababu nomino zote hutangulizwa na irabu kwa kuwa lugha ya Ekegusii ni chopekezi inapendelea kuchopeka irabu mwanzoni mwa maneno .

Mifano ni kama ifuatavyo:

18. Ekegusii	Fasiri
---------------------	---------------

- | | |
|----------------------|--------|
| (a) /□\$m□\$nt□/ | mtu |
| (b) /□\$sa\$ni/ | sahani |
| (c) /□\$g□\$ta\$βu/ | kitabu |

2.4.2.5 Muundo wa konsonanti irabu irabu(KII)

Huu ni muundo ambao hutokea ambapo konsonanti hufuatwa na irabu mbili. Mfuatano huu wa irabu aghalabu hudhihirika kama irabu ndefu. Katika muundo huu nafasi ya kwanza huchukuliwa na konsonanti kisha hufuatwa na irabu ya aina moja mara mbili. Muundo huu hauna maneno mengi katika Ekegusii. Aghalabu maneno yaliyokopwa hupokezwa irabu ndefu. Kwa mfano;

19.	Ekegusii	Fasiri
	(a) /re:ro/	leo
	(b) /□bu:ku/	bibilia

2.4.3 Ulinganuzi wa miundo ya silabi za Kiswahili sanifu na Ekegusii

Lugha hizi mbili zina asili moja kwani zote ni za Kibantu. Japo miundo ya silabi imeonekana kuwiana kwa kiwango kikubwa, kuna tofauti inayodhihirika katika baadhi ya miundo fulani. Hata hivyo hakuna lugha zinazofanana katika kila hali. Katika lugha hizi mbili kuna muundo wa silabi uliopendelewa nao ni konsonanti na irabu. Muundo huu umejidhihirisha pakubwa sana katika lugha hizi mbili. Hata hivyo kuna miundo fulani inayopatikana katika Kiswahili lakini haipatikani katika Ekegusii. Nayo ni:

Kwanza ni muundo wa silabi ya konsonanti pekee unaojitokeza katika lugha ya Kiswahili lakini katika lugha ya Ekegusii haupo. Katika lugha ya Kiswahili aghalabu muundo huu unapatikana katika maneno yaliyokopwa lakini maneno yaliyokopwa katika Ekegusii yanaendelezwa yakifuata kanuni za lugha ya Ekegusii kwa hivyo ni vigumu kupata muundo huu. Isitoshe, maneno asilia ya Ekegusii hayana muundo huu. Mathalani neno ‘skuli’ lina muundo wa silabi ya konsonanti pekee katika Kiswahili lakini katika lugha ya Ekegusii linaendelezwa ‘esukuru’. Mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili na lugha yake ya kwanza ikiwa ni Ekegusii ataliendeleza kama ‘sikuli’ ili kutimiza masharti ya silabi pendwa. Mwanafunzi hufanya hivi kwa sababu katika lugha yake ya mama hakuna muundo huu kwa hivyo atajaribu kuhamisha kanuni za lugha ya kwanza katika matumizi ya lugha ya pili.

Muundo mwingine ni wa KKKI ambao pia haupo katika lugha ya Ekegusii japo upo katika Kiswahili. Muundo huu pia unapatikana katika maneno yaliyokopwa kutoka lugha zingine kwenda Kiswahili .

Muundo wa KKYI unajitokeza katika lugha ya Kiswahili japo katika maneno machache sana. Lakini katika lugha ya Ekegusii haupo.

2.5 Hitimisho

Lugha ya Kiswahili na Ekegusii zinafanana kwa kuzingatia miundo ya silabi kwa kuwa zote ni lugha za kibantu zilizo na mifumo ya sauti inayokaribiana kutokana na ukweli kuwa zinatokana na mame Bantu, lakini kuna tofauti za miundo ya silabi japo si nyingi. Kama tulivyotaja hapo juu, kuna baadhi ya miundo ya silabi inayopatikana katika lugha ya Kiswahili lakini haipatikani katika lugha ya Ekegusii. Tofauti hii inachangia katika baadhi ya

makosa ya miundo isiyofaa katika lugha ya Kiswahili. Mathalani tumetaja kuwa lugha ya Ekegusii haina muundo wa silabi wa konsonanti pekee lakini katika lugha ya Kiswahili kuna muundo huu. Katika uchanganuzi wa data tulipata kuwa baadhi ya wanafunzi waliendeleza maneno ya Kiswahili yaliyo na muundo huu visivyo. Kwa mfano waliandika neno ‘skuli’ kama ‘sikuli’. Wao hulazimika kuyaendeleza maneno haya kwa kufuata muundo wa konsonanti irabu unaopatikana katika lugha yao ya kwanza.

SURA YA TATU

3.0 UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA

3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia na ya kimofolojia pamoja na kueleza sababu zilizowapelekea wanafunzi kufanya makosa haya. Makosa yameorodheshwa na kupangwa katika makundi tofauti na sehemu ambamo yanapatikana. Makosa haya yameainishwa baada ya insha za wanafunzi kusahihishwa ili kubaini makosa ya kifonolojia na ya kimofolojia kama yalivyojitokeza kutokana na data tuliyokusanya. Makosa haya ni yale yanayodhihirika miongoni mwa wazungumzaji wa Ekegusii wanapotumia lugha ya Kiswahili hasa katika maandishi. Makosa mengine yaliyojitokeza na ambayo hayakuhusu tatizo la utafiti yalipuuzwa. Makosa haya ni kama vile ya msamiati, mtindo, uakifishaji, n.k. Hii ni kwa sababu upeo wa tatizo la utafiti huu ni uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia bali si makosa mengine yanayotokana na kategoria zingine.

Katika sura iliyotangulia tumetoa ufanuzi kuhusu lugha hizi mbili. Kwa kiasi kikubwa tumeona kufanana na pia kutofautiana kwa lugha hizi mbili. Mathalani tumeainisha fonimu za lugha hizi na kupata kuwa hata kama lugha hizi ni za nasaba moja zinatofautiana kifonimu; baadhi ya fonimu zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili hakipatikani katika lugha ya Ekegusii. Aidha baadhi ya zile zinazopatikana katika lugha ya Ekegusii hazipatikani

katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na kutofautiana kifonimu na kimuundo katika baadhi ya maneno, wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii huathirika pakubwa sana wanapotumia lugha ya Kiswahili kama ilivyojidhihirisha kutokana na data tuliyokusanya.

Baada ya kuyaainisha makosa na kuyaweka katika kategoria tofauti, tulitoa visabibishi nya makosa hayo. Kila lugha huwa na mfumo wake maalumu unaofaa kufuatwa katika uundaji wa maneno. Ikiwa mfumo huo hautafuatwa basi lugha hiyo itakuwa imetumiwa visivyo. Aghalabu wazungumzaji wa Ekegusii huhamisha mifumo ya lugha yao wanapotumia Kiswahili na kupata maumbo yasiyo sahihi. Hii husababisha utata wa maana na wakati mwengine hata maana iliyokusudiwa kupotea kabisa.

Katika uchanganuzi wa makosa haya tuliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Corder. Kwa mujibu wa Corder (1974), mtafiti hifuata hatua zifuatazo katika uchanganuzi makosa:

1. Kukusanya sampuli ya wanaojifunza lugha.
2. Kutambua makosa.
3. Kueleza makosa kwa kuyaweka katika makundi.
4. Kufafanua visababishi nya makosa hayo.
5. Kutathmini makosa haya.

3.2 Makosa ya kifonolojia

Tunapochunguza fonolojia ya Ekegusii na Kiswahili Sanifu tunagundua kuwa lugha hizi mbili zinaingiliana pakubwa sana. Kuingiliana huku husababisha ukiukaji wa kanuni za

kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo. Makosa haya hutokea wakati mwanafunzi anapohamisha sauti aliyooizoea katika lugha yake ya kwanza kwenda lugha ya Kiswahili. Wakati mwingine wao huchanganya matumizi ya sauti kwa sababu ya kuathirika na lugha ya Kwanza. Wanafunzi hutatizika sana kwa sababu fonimu walizozizoea katika lugha ya Ekegusii hazipatikani katika lugha ya Kiswahili au zile zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili hazipatikani katika lugha ya Ekegusii. Baadhi ya makosa ya kifonolojia ni:

3.2.1 Matumizi ya /r/ badala ya /l/

Baadhi ya wazungumzaji wa Ekegusii hutumia fonimu /r/ badala ya /l/ au badala ya kutumia /r/ wao hutumia fonimu /l/. Kwa mfano:

20. (i)a*-----nilipokuwa nikienderea na safari yangu-----
 (i)b-----nilipokuwa nikiendelea na safari yangu-----
 (ii)a*-----aliniambia turudi na yeze tuwe tukiangaria-----
 (ii)b-----aliniambia turudi naye tuwe tukiangalia-----
 (iii)a* Tangu siku hiyo sitasahau niliyoyasikia na kuyaona baadaye kuwa ya kweli.
 (iii)b Tangu siku hiyo sitasahau niliyoyasikia na kuyaona kuwa ya kweli.
 (iv)a *Nilijalibu kupiga kelele lakini sauti yangu haikunitoka.
 (iv)b Nilijaribu kupiga kelele lakini sauti yangu haikunitoka.

Ekegusii hakina fonimu /l/. Kwa sababu hii wanafunzi wengi hukanganyika wasijue jinsi ya kutumia fonimu hizi mbili ipasavyo. Wao hutumia fonimu /l/ mahali pa /r/ au /r/ badala ya /l/. Mwanafunzi anapojifunza Kiswahili inamlazimu kujifunza fonimu /l/ isiyopatikana katika lugha yake ya kwanza. Mara nyingi wanafunzi wengi hukosa kutofautisha fonimu hizi

mbili na hili hutokana na athari ya L1. Matatizo hutokea wakati sauti aliyoizoea mwanafunzi katika lugha yake ya kwanza huwa haipatikani katika lugha ya Kiswahili. Hivyo mwanafunzi atatamka iliyo karibu nayo. Katika mifano iliyoko hapo juu, mwanafunzi ametumia fonimu /r/ badala ya /l/ na mahali alipaswa kutumia fonimu /r/ ametumia /l/. Ameandika ‘nikienderea’ badala ya ‘nikiendelea’, ‘nilijalibu’ badala ya ‘nilijaribu’.

3.2.2 Matumizi ya /ʃ/ badala ya /tʃ/

Baadhi ya wanafunzi huchanganya matumizi ya sauti /ʃ/ na /tʃ/ kwa sababu sauti /ʃ/ ya Kiswahili haipatikani katika lugha ya Ekegusii. Mwanafunzi hushawishika kutumia sauti inayokaribiana nayo. Kwa mfano:

21. (i)a* Nilishtuka na kuanguka jini.
 - (i)b Nilishtuka na kuanguka chini.
 - (ii)a* Usingizi ulinijukua bila kujua-----
 - (ii)b Usingizi ulinichukua bila kujua-----
 - (iii)a* Papo hapo nilikuwa na usingizi jungu nzima.
 - (iii)b Papo hapo nilikuwa na usingizi chungu nzima.

Pia kuna matumizi ya /tʃ/ badala ya /ʃ/. Kwa mfano:

- (iv) a*-----sichui vile mwizi huyo alitoroka.
- (iv) b----- sijui vile mwizi huyo alitoroka.
- (v) a* Nilichinyatua hadi inche nilichalibu juu chini hadi nikatafuta mti nakupanda juu.
- (v) b Nilijinyatua hadi nje, nilijaribu juu chini hadi nikatafuta mti na kupanda juu.

Katika lugha ya Ekegusii hakuna fonimu /ʃ/, badala yake kuna fonimu /tʃ/. Fonimu hii ndiyo hutumiwa na baadhi ya wanafunzi mahali pa /ʃ/

3.2.3 Matumizi ya /s/ badala ya /z/

Mfumo wa fonimu wa Ekegusii hauna sauti /z/. Mzungumzaji wa Ekegusii anapotumia Kiswahili hutumia sauti /s/ badala ya /z/. Mifano:

22. (i) a* Hapo sama za sama palikuwepo na mzee mmoja.
(i) b Hapo zama za zama palikuwepo na mzee mmoja.
(ii) a*. Huyo mzee aliniulisa vizuri sana-----
(ii) b Huyo mzee aliniuliza vizuri sana-----
(iii) a* Walifurahi kuwa wamepata mtumishi wa kufanya kasi.
(iii) b Walifurahi kupata mtumishi wa kufanya kazi.

Lugha ya Ekegusii haina fonimu /z/ badala yake kuna fonimu /s/. Baadhi ya wazungumzaji wa Ekegusii wanapotumia lugha ya Kiswahili hutumia sauti /s/ badala ya /z/ kwa sababu ya kuathirika na L1. Wao hutumia fonimu inayokaribiana na fonimu /z/.

3.2.4 Matumizi ya /s/ badala ya /ʃ/

Fonimu /ʃ/ haipatikani katika Ekegusii. Fonimu inayokaribiana nayo kimatamshi ni /s/. Wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii huathirika na lugha ya kwanza wanapotumia sauti hii. Mifano:

23. (i) a*----nilisikwa na jitu huyo akanipeleka mahali anakoishi.
(i) b----nilishikwa na jitu hilo likanipeleka mahali linakoishi
(ii) a* Wakati mama alitoka safarini alipata nemesakula.

- (ii) b Wakati mama alitoka safarini alipata nimeshakula.
- (iii) a * Nilisangaa sana kuona jinsi tulivamiwa na majambazi.
- (iii) b Nilishangaa sana kuona jinsi tulivamiwa na majambazi.

Ekegusii hakina fonimu /ʃ/ badala yake kuna fonimu /s/. Mwanafunzi aliyezoea fonimu /s/ katika lugha yake ya kwanza huathirika anapotumia sauti hii kwa hivyo yeye hutumia sauti inayokaribiana nayo.

3.2.5 Matumizi ya /p/ badala ya /b/

Fonimu /p/ na /b/ hazipatikani katika lugha ya Ekegusii. Badala yake, sauti /β/ iliyo kikwamizwa ndiyo inayopatikana. Wanafunzi hutatizika wasijue fonimu ya kutumia. Mifano:

24. (i) a* Yule mzee aliwaambia askari kuwa huyu mtoto ameniipia
- (i) b Yule mzee aliwaambia askari kuwa huyu mtoto ameniibia.
 - (ii) a* Walikuwa wamejificha na pastola zao.
 - (ii) b Walikuwa wamejificha na bastola zao.
 - (iii) a* Ni ukweli wahenga walisema pendera hufuata upepo.
 - (iii) b Ni ukweli wahenga walisema bendera hufuata upepo

3.2.6 Matumizi ya /b/ badala ya /p/

Kama tulivyotaja hapo juu fonimu hizi hazipatikani katika lugha ya Ekegusii. Mifano ya makosa yanoyotokana na athari za fonimu hizi ni:

25. (i) a* Bunde si bunde nilijibata mikononi mwa jitu.

- (i) b Punde si punde nilijipata mikononi mwa jitu.
- (ii) a* Bamoja tuliandamana hadi kituo cha polizi.
- (ii) b Pamoja tuliandamana hadi kituo cha polisi.
- (iii) a* Ilikuwa ni siku ya Jumabili mwaka wa elfu mbili na kumi na nne.
- (iii) b Ilikuwa ni siku ya Jumapili mwaka wa elfu mbili na kumi na nne.

Katika fonimu za Ekegusii hakuna fonimu /b/ na /p/ zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili. Fonimu hizi ni vipasuo visivyopatikana katika lugha ya Ekegusii badala yake kikwamizwa /β/ ndicho kinachopatikana ambacho hakipo katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hushindwa kutumia fonimu hizi na mara kwa mara fonimu hizi hubadilishana nafasi.

3.3. Makosa ya Kimofolojia

Mofolojia ni taaluma ya isimu ambayo huchunguza maumbo ya maneno na hususan maumbo ya mofu. Maumbo ya maneno huweza kuathiri uteuzi wa viambishi-vipatanishi katika sentensi kama tutakavyoona katika sehemu ya makosa ya kisintaksia. Makosa katika kiwango cha mofolojia yamejitokeza katika miundo ya maneno isiyo sahihi hasa katika ngeli ya 1 na 3. Katika Kiswahili irabu /u/ hudondoshwa katika nomino za ngeli hizi. Ilhahi udondoshaji huu haujitokezi katika lugha ya Ekegusii. Pia kuna yale yaliyohusu kuongeza kwa kiambishi katika nomino isiyokuwa na kiambishi hicho na kwingine kuacha kiambishi kinachoashiria dhana fulani kama vile wingi. Baadhi ya mifano tuliyopata ni kama ifuatayo:

3.3.1 Uchopekaji wa irabu /u/

Tofauti na jinsi ilivyo katika Kiswahili ambapo maneno mengi huyeyusha /u/ na kuwa /w/ inapofuatwa na irabu nyingine isipokuwa /i/. Maneno mengi katika Ekegusii huwa na fonimu /u/. Mifano:

26. (i) a* Nilishangaa sana kwa nini nilikuwa kama mulevi.
 - (i) b Nilishangaa sana kwa nini nilikuwa kama mlevi.
 - (ii) a* Hapo nilichelewa kuamuka-----
 - (ii) b Hapo nilichelewa kuamka-----
 - (iii) a* Mimi na wazazi wangu tuliponea tu kwa kusalimu amuri
 - (iii) b Mimi na wazazi wangu tuliponea tu kwa kusalimu amri.

Lugha ya Kiswahili hudondosha irabu /u/ katika ngeli ya 1, 2 na 3 pale ambapo irabu mbili zinafuatana au inapotanguliwa na kiambishi cha ngeli na kufuatwa na konsonanti nyingine. Udondoshaji wa irabu hutokea ili kusahilisha matamishi na pia kupata muundo ufaao ili kuepuka uziada. Lugha ya Ekegusii haidondoshi irabu /u/ katika ngeli ya 1, 2 na 3. Nomino katika ngeli hii husalia na irabu hiyo kwa hivyo wazungumzaji wa Ekegusii huhamisha miundo ya maneno katika ngeli hizi katika lugha ya Kiswahili.

3.3.2 Udondoshaji wa sauti /h/

Wanafunzi wengi walidondo sauti /h/ katika baadhi ya maneno na walipokanusha kauli tofauti. Kwa mfano:

27. (i) a* Niliamka asubui na mapema-----
(i) b Niliamka asubuhi na mapema-----

(ii) a* Walimchapa wakamwacha hoe hae.
(ii) b Walimchapa wakamwacha hohehahe.
(iii) a* Alijiunga na kundi la wezi kwa sababu alikuwa ayatii maoni aliyopewa na wazazi wake.
(iii) b Alijiunga na kundi la wezi kwa sababu alikuwa hayatii maoni aliyopewa na wazazi wake.

Baadhi ya makosa mengine yalikuwa ni uchopekaji wa fonimu /h/ mahali kusipofaa. Kwa mfano:

28. (i) a*-----nilisikia mbwa akibweka hovyo hovyo.
(i) b-----nilisikia mbwa akibweka ovyoovyo.
(ii) a* Baada ya kuokolewa na msamalia mwema nilimwambia hasante.
(ii) b Baada ya kuokolewa na msamaria mwema nilimwambia asante.
(iii) a* Tukiwa kule hangani nikaota kuwa ndege amebotesa mwelekeo.
(iii) b Tukiwa kule angani niliota kuwa ndege imepoteza mwelekeo.

Ekegusii hakina fonimu /h/, kwa sababu hii baadhi ya wazungumzaji wa lugha hii huidondosha au huichopeka fonimu hii mahali kusikofaa. Hii husababisha kupatikana kwa miundo isiyokubalika ya lugha ya Kiswahili. Sentensi inapokanushwa aghalabu sauti /h/ hutumiwa katika ukarushaji, wanafunzi huidondoa fonimu hii katika ukarushaji. Fonimu /h/ hutumiwa pamoja na kiambishi kikanushi katika kukanusha nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi. Mathalani hukanusha sentensi “Mtajutia makosa yenu.” Kama “Amtajutia makosa yenu.” Badala ya “Hamtajutia makosa yenu.”

3.3.3 Uyeyushaji

Makosa mengine yaliyopatikana ni kukosa kuyeyusha irabu na kuwa kiyeyusho. Katika uyeyushaji, irabu /i/ hubadilika na kuwa kiyeyusho /y/ ilhali irabu /u/ hubadilika na kuwa kiyeyusho /w/. Sababu hasa huwa ni kuepuka ufuatanaji wa irabu mbili. Pia kuunda muundo wa silabi uliopendelewa. Kwa mfano:

29. (i) a*. Mualimu alituhimiza kufanya bidii masomoni.
 - (i) b. Mwalimu alituhimiza kufanya bidii masomoni.
 - (ii) a*. Muizi huyo alijalibu kutoroka lakini alikamatwa na wanakijiji waliokuwa na hasira kubwa.
 - (ii) b. Mwizi huyo alijaribu kutoroka lakini alikamatwa na wanakijiji waliokuwa na hasira kubwa.
 - (iii) a*. Wezi walituvamia kuetu nyumbani.
 - (iii) b. Wezi walituvamia kwetu nyumbani.

Wanafunzi walikosa kuyeyusha irabu /u/ ili kupata kiyeyusho /w/. Hili lilosababisha kupatikana kwa miundo ya maneno isiyo sahihi.

3.3.4 Muundo wa silabi usiofaa

Miundo ya maneno katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii ni tofauti. Katika lugha ya Kiswahili kuna muundo wa silabi wa konsonanti pekee lakini muundo huu haupatikani katika lugha ya Ekegusii. Tofauti hii huathiri matumizi ya Kiswahili kwa kiwango fulani. Kuna pia muundo wa konsonanti konsonanti kosonanti irabu (KKKI) unaopatikana katika lugha ya

Kiswahili lakini haupatikani katika lugha ya Ekegusii. Mifano ya maneno yaliyo na muundo huu ni:

30. (i) a* ---baada ya kimia cha dakika tatu-----
(i) b.----baada ya kimya cha dakika tatu-----
(ii) a*. Huyu mtu alikuwa ni Mwfirika-----
(ii) b. Huyu mtu alikuwa ni Mwfrika-----
(iii) a*. Mimi na wazazi wangu tuliponea kwa kusalimu amuri.
(iii) b. Mimi na wazazi wangu tuliponea kwa sababu tulisalimu amri.

Muundo wa silabi ya konsonanti pekee unaojitokeza katika lugha ya Kiswahili haupatikani katika lugha ya Ekegusii. Aghalabu katika lugha ya Kiswahili muundo huu unapatikana katika maneno yaliyokopwa lakini maneno yaliyokopwa katika lugha ya Ekegusii yanaendelezwa yakifuata kanuni za lugha hiyo kwa hivyo ni vigumu kupata muundo huu. Pia katika maneno asilia ya Ekegusii hakuna muundo huu. Mathalani, mwanafunzi ameandika ‘mwfirika’ badala ya ‘mwafrika’ muundo wa silabi wa neno mwafrika ni: /mwa\$f\$ri\$ka/. Silabi {f} haina irabu. Mwanafunzi huiongezea silabi hii irabu kwa sababu katika lugha yake ya kwanza hakuna maneno yaliyo na muundo huu. Kwa sababu hii, wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii huathirika pakubwa sana wanapokumbana na maneno ya Kiswahili yaliyo na muundo huu. Wao hulazimika kuyaendeleza maneno haya kwa kufuata muundo wa konsonanti irabu (KI) unaopatikana katika lugha yao ya kwanza.

3.4 Hitimisho

Sababu za makosa mengi kutokea ni kuathiriwa na lugha ya kwanza. Wanafunzi wengi hutatizwa na L1 na hili huchangia katika baadhi ya makosa yanayofanywa katika harakati za

kujifunza L2. Hii ni kwa sababu wakati mwanafunzi anapojieleza katika lugha lengwa, atarejelea lugha ambayo anaifahamu vizuri na ambayo ni L1. Mwanafunzi atahamisha kanuni kutoka L1 hadi L2. Makosa haya yanayofanywa hufanana na sifa za L1 na hivyo utapata kuwa baadhi ya makosa yametafsiriwa moja kwa moja kutoka L1. Hivyo mitindo ya L1 huwa muhimu kwa sababu huwa kama msingi wa sarufi za kwanza za wanaojifunza L2. Kwa sababu hii, kuingiliana kwa lugha ni sababu mojawapo inayochangia wanafunzi kufanya makosa haya.

Sababu nyingine iliyochangia kutokea kwa makosa haya ni ufundishaji mbaya kutokana na uelewa mbaya wa mwalimu. Walimu wengi wa Kiswahili sio wazawa wa lugha ya Kiswahili, wamejifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Wakati mwingine mwalimu na mwanafunzi huwa na lugha ya kwanza tofauti, kwa hivyo si rahisi mwalimu kuelewa ugumu alionao mwanafunzi. Huenda ukapata mwalimu naye ameathirika na lugha yake ya kwanza. Kwa sababu mwanafunzi hujifunza lugha kwa kumsikiza mwalimu wake anavyozungumza, wanaposikia matamshi mabaya kutoka kwa mwalimu nao hufanya makosa yayo hayo. Mwanafunzi haelewi kuwa mwalimu amefanya makosa, yeye huyachukua makosa yale na kuyachukulia kama maumbo sahihi, hufanya hivi kwa kusahilisha sarufi ili kufikia uamilifu mpana wa mawasiliano. Kwa mfano, mwanafunzi ameandika ‘hio hio’ badala ya ‘hiyo hiyo’. Mwanafunzi amedondosha fonimu /y/ ili kurahisisha matamshi. Fonimu /y/ hutumia nguvu nyingi kutamkwa ikilinganishwa irabu /ɔ/.

Tukizingatia uainishaji wa ngeli kimofolojia, maneno mengi ya Ekegusii ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili hupatikana katika ngeli tofauti. Kwa hivyo, wazungumzaji wa Ekegusii huzingatia kiambishi awali katika kuunda sentensi na wanapohamisha matumizi haya katika Kiswahili, hufanya makosa. Katika hali hii wanafunzi wanajumuisha makosa kwa kuhamisha kanuni za lugha ya kwanza. Isitoshe, tumegundua kuwa kuna tofauti kati ya miundo ya

maneno ya lugha hizi mbili. Tofauti hizo huathiri matumizi ya Kiswahili kwa kiwango fulani. Kwa mfano, katika lugha ya Kiswahili maneno ya ngeli ya kwanza na ya pili hudondosha irabu /u/ lakini katika Ekegusii irabu /u/ haidondoshwi katika ngeli ya kwanza na ya pili. Kwa hivyo nomino za ngeli ya kwanza na ya pili husalia na sauti hiyo. Wazungumzaji wa Ekegusii hufanya makosa ya kuhamisha matumizi ya nomino za ngeli ya kwanza na pili katika Kiswahili.

SURA YA NNE

4.0 UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KISINTAKSIA

4.1 Utangulizi

Kutokana na data tuliokusanya makosa mengi yaliyojitokeza ni ya kisintaksia. Makosa haya hutokea pale ambapo upatanisho wa kisarufi haujazingatiwa. Upatanisho wa kisarufi ni ule uwiano unaopatikana baina ya nomino na maneno mengine katika sentensi. Kiambishi kinachoambishwa katika kitenzi ni kile kinachofungamana na ngeli ya nomino husika. Nomino hii ni ile iliyo na uamilifu wa kiima. Kiswahili ni lugha ambishibainishi hivyo kuna mwingiliano mkubwa wa mofolojia yake na sintaksia. Mwingiliano huu hubainika wazi hasa katika upatanisho wa kisarufi. Nomino ndio msingi wa upatanisho katika sentensi kwani ndio huamua viambishi vya upatanisho. Nomino hizi hukubaliana kiadadi, katika ngeli na vipengele vingine katika sentensi kama vile vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Nomino inapobadilika katika sentensi, viambishi vya upatanisho navyo hubadilika. Kwa mfano:

31. Mama **alimchapa** Moraa **alipoangusha** kikombe **kikavunjika**.

Katika mfano huu, nomino mama na Moraa ziko katika ngeli ya A-WA na ndiyo sababu kiambishi **a** kimepachikwa mwanzoni mwa kitenzi lakini nomino kikombe iko katika ngeli ya KI-VI ndiposa kiambishi **ki** kimepachikwa mwanzoni mwa kitenzi. Ni ukweli kuwa nomino inapobadilika kiambishi cha upatanisho nacho hubadilika. Kwa hivyo nomino ndiyo inayotawala aina ya kiambishi kinachoambishwa katika sentensi.

Upatanisho pia huashiriwa na viambishi vya nafsi. Viwakilishi vya nafsi hubainishwa katika ngeli ya kwanza na ya pili. Kuna nafsi tatu katika lugha ya Kiswahili sanifu, nafsi hizi zina viambishi tofauti kama inavyojidhihirisha katika maelezo yafuatayo.

Nafsi ya kwanza huwakilishwa na kiwakilishi **mimi** katika hali ya umoja na **sisi** katika hali ya wingi. Viambishi vinavyowakilisha nafsi hii katika umoja na wingi ni **ni-** na **tu-**. Nafsi ya pili huwakilishwa na kiwakilishi **wewe** katika umoja na **ninyi / nyinyi** katika wingi. Viambishi viwakilishi nya nafsi hii ni **u-** na **m-** katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Viwakilishi **yeye** na **wao** huwakilisha nafsi ya tatu. Viambishi viwakilishi nya nafsi hii ni **a-** katika umoja na **wa-** katika wingi. Viambishi hivi ndivyo huashiria upatanisho wa kisarufi.

Mfano katika sentensi:

32. Umoja	Wingi
(i) Ninampenda Daniel sana.	Tunampenda Daniel sana.
(ii) Unampenda Daniel sana.	Mnampenda Daniel sana.
(iii) Anampenda Daniel sana.	Wanampenda Daniel sana.

Vitenzi nya Kiswahili sanifu huchukua upatanisho wa kiima kulingana na ngeli ya Kikundi Nomino chake. Kiambishi hiki aghalabu huwa ni cha kwanza. Kiambishi hiki ni cha lazima katika mofolojia ya kitenzi cha Kiswahili sanifu. Upatanisho pia hudhihirika katika kuonyesha uambishaji wa urejeshi. Uambishi huu hudhihirika katika kitenzi. Kiambishi cha urejeshi huonyesha upatanisho na kiima kinachorejelewa. Viambishi nya urejeshi ni tofauti na nya kiima ingawa navyo pia hutegemea ngeli. Isitoshe, viambishi nya upatanisho wa yambwa tendwa pia huambishwa kwenye vitenzi nya Kiswahili sanifu. Viambishi hivi sawa na nya kiima na hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

Kwa mujibu wa maelezo haya tumeweza kubainisha kwamba katika Kiswahili sanifu upatanisho huathiriwa na ngeli ya nomino husika. Nomino inayotumika kama kiima ndiyo ambayo hutuelekeza katika viambishi vitakavyoambikwa katika maneno mengine yanayofuata katika kikundi nomino. Ngeli ya nomino huathiri upatanisho wa viwakilishi,

vivumishi na vitenzi katika sentensi. Uelewa huu ndio tuliotumia katika kuchanganua makosa katika insha za wanafunzi walizozilandika. Tumezingatia jinsi wanafunzi wameunganisha maneno katika sentensi na kuona ikiwa walizingatia kanuni za Kiswahili sanifu. Suala la upatanishi ni la kisintaksia kwa sababu linavuka mipaka ya neno moja. Upatanishi huhusisha angalau maneno mawili au zaidi. Makosa mengi zaidi yalijitokeza katika sehemu ya kira-tenzi kwa sababu ya kitenzi cha Kiswahili kina uwezo wa kuchukua viambishi tofauti vinavyowakilisha dhana mbalimbali. Baadhi ya makosa tuliyopata ni yale yaliyokiuka kanuni za upatanishi.

4. 2 Mifano ya makosa ya kisintaksia

Makosa ya kisintaksia hutokea pale ambapo hakuna upatanisho wa kisarufi. Mwanafunzi hana budi kuteua viambishi vipatanishi sahihi anapotunga sentensi. Uteuzi wa vipatanishi vy a ngeli mbalimbali hutegemea jinsi nomino husika ilivyoainishwa. Nomino inapoainishwa katika ngeli fulani hutumia vipatanishi vy a ngeli hiyo. Mfano nomino ‘maiti’ inapoainishwa katika ngeli ya kwanza, huchukua upatanisho wa ngeli hiyo amba ni ‘a-‘ katika umoja na ‘wa-‘ katika wingi. Lakini nomino hii inapoainishwa katika ngeli ya tisa huchukua upatanisho wa ngeli hiyo, amba ni ‘i-‘ katika umoja na ‘zi-‘ katika wingi.

Ni vigumu kuvitumia kigezo zaidi ya kimoja kwa pamoja katika kuainisha ngeli. Kutumia vigezo hivi kwa pamoja kunaweza kuzua utata, pale ambapo nomino fulani inaweza kuingizwa katika ngeli tofauti tofauti. Mathalani, uainishaji kimofolojia uainisha nomino kwa kutumia sura za maumbo yenyewe. Katika uainishaji huu nomino kama vile: kit, kilema, kifaranga, kijiko hujumuishwa pamoja katika ngeli ya saba. Udhaifu wa uainishaji huu ni kuwa hauzingatii ukweli kuwa ziko nomino zenye sifa za kimofolojia zinazofanana lakini

ambazo haziwezi kutiwa katika kundi moja. Kwa mfano, ingawa nomino kilema na kifaranga zinafanana kimofolojia na nomino zingine katika kundi hili, haziwezi kuainishwa pamoja kwa sababu nomino hizi zina uhai ilhali nomino katika ngeli ya saba hazina uhai. Uainishaji huu unaweza kuchangia kosa la uteuzi wa kipatanishi ‘ki-‘ kwa nomino kilema na kifaranga, badala ya kipatanishi ‘a-‘. Uainishaji huu unaweza kutumiwa kuainisha nomino kama kijiko, kitii, na kikombe kwenye ngeli ya saba. Lakini nomino kifaranga na kilema zinfaa kuainishwa kwa kutumia kigezo cha kisemantiki.

Makosa mengi yaliyojitekeza katika sehemu hii yalihusu ngeli na upatanishi wake kisarufi. Hapa ndipo dhana za mafolojia na sintaksia zilipodhihirika wazi.

4.2.1 Ukiushi wa viambishi vyta nafsi

Viambishi viwakilishi vya nafsi huashiria upatanisho wa kisarufi. Viwakilishi hivi hubainishwa katika ngeli za kwanza na pili. Mifano ya makosa yaliyotokana na ukiushi wa nafsi ni:

33. (i) a*. Nalikuwa na nyiwele nyeusi tititi kama makaa.
(i) b. Nilikuwa na nywele nyeusi tititi kama makaa.
(ii) a*. Nalikuwa naelekea kitandani kulala usingizi ulinishika nakalala fofoto.
(ii) b. Nilikuwa naelekea kitandani kulala usingizi uliponishika nikalala fofoto.
(iii) a*. Ilifika siku ya kurudi nyumbani naliaza safari yangu saa kumi anusu nalipanda ndege.
(iii) b. Ilifika siku ya kurudi nyumbani, nikaanza safari yangu saa kumi unusu, nikapanda ndege.

Katika mifano iliyo hapo juu wanafunzi wametumia kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza vibaya. Badala ya mwanafunzi kutumia kiambishi “ni” anatumia kiambishi “na”.

Mfano mwanafunzi ameandika ‘nalikuwa’ badala ya ‘nilikuwa’, katika lugha yake ya Ekegusii kiambishi ‘na’ hutumiwa kutajia matukio yanayofuatana. Sababu inayochangia kosa hili ni ujumlishaji mno pamoja na kutolewa kanuni za lugha lengwa. Mwanafunzi alihamisha kanuni za lugha yake ya kwanza na kuzilazimisha katika lugha ya Kiswahili.

4.2.2 Matumizi mabaya ya vivumishi

Vivumishi ni maneno yanayoeleza zaidi juu ya nomino au kiwakilishi chake. Kivumishi kinaweza kutoa maelezo kuhusu jinsi jina linalotajwa liliyvo, tabia ya jina hilo, mahali au idadi ya majina, n.k.. Vivumishi hutumika pamoja na nomino kama viambajengo vya kikundi nomino. Vivumishi hivi kimundo, huathiriwa na aina ya nomino inayohusika. Viambishi vipatanishi hivyo huonyesha upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi. Ikiwa mwanafunzi hatateua vipatanishi sahihi atakuwa amefanya kosa la kisarufi. Baadhi ya vivumishi hasa vile vya mkopo havichukui viambishi vyovyyote. Ngeli ambamo nomino fulani hupatikana ndiyo ambayo hutuongoza kuamua viambishi vitakavyoambishwa kwenye mzizi wa kivumishi kinachovumishwa. Kuna aina tofauti tofauti za vivumishi, makosa ya uambishaji usiofaa yalifanywa katika aina hizi tofauti. Baadhi ya makosa tuliyopata ni kama vile:

34. (i) a*. Jambazi ambaye aliyepigwa mawe alikufa.
 - (i) b. Jambazi ambaye alipigwa mawe alikufa. Au
 - (i) c. Jambazi aliyepiwa mawe alikufa.
- (ii) a*. Siku hiyo ya arusi nilijikwatua nikawa msafi sana.
- (ii) b. Siku hiyo ya arusi nilijikwatua nikawa safi sana.
- (iii) a*. Nilikula chakula yangu nikamaliza.
- (iii) b. Nilikula chakula changu nikamaliza.

(iv) a*. Wavulana wasita walitokea ghafla.

(iv) b. Wavulana sita walitokea ghafla.

Vivumishi virejeshi amba- na ‘o’ rejeshi havistahili kufuatana katika sentensi kurejelea nomino moja. Mwanafunzi ametumia virejeshi amba- na ‘o’ kurejelea nomino jambazi. Mwanafunzi alikosa kubaini kuwa virejeshi hivi havitumiwi katika sentensi kurejelea nomino moja. Vivumishi nya sifa hueleza sifa au tabia za nomino husika, kuna vivumishi nya sifa ambavyo huongezewa viambishi tofauti tofauti kutegemea ngeli husika. Pia kuna vile ambavyo haviongezwi viambishi vyovyote katika ngeli zote. Aghalabu vivumishi hivi ni maneno ya mkopo. Kivumishi ‘safi’ hakiongezewi viambishi vyovyote. Vivumishi vimilikishi huambishwa viambishi nya ngeli kutegemea nomino ili kutoa maana inayokusudiwa. Nomino chakula iko katika ngeli ya KI-VI, mwanafunzi anapoambisha kiambishi katika mzizi wa kivumishi kimilikishi –angu inampasa kuzingatia nomino husika kwa hivyo badala ya kusema ‘chakula yangu’ angesema ‘chakula changu’.

Mbali na ujumlishaji mno wa sheria za ngeli moja hadi nyingine, kuna kule kutumia sheria mahali kusikofaa. Tunaelewa kuwa wanafunzi hawa wamefunzwa kuhusu ngeli na upatanishi wake kisarufi. Mwanafunzi anaposema ‘wavulana wasita’ badala ya ‘wavulana sita’ anaelewa kuwa nomino wavulana inapatikana katika ngeli ya A-WA, hivyo kiambishi cha kipatanishi cha wingi ni ‘wa-’. Hivyo kusema ‘wavulana wasita’ bila ya kuelewa kuwa kivumishi cha idadi ‘sita’ hakiambwii kwa vyovyote vile hata katika hali ya umoja au wingi.

4.2.3 Ukiushi wa kiambishi cha ‘-a’ unganifu.

Kiambishi hiki cha ‘-a’ unganifu hutumiwa na kiambishi cha ngeli pamoja na kihuishi au nomino kuunda kivumishi. ‘-a’ unganifu ni kiambishi tamati kinachoambatishwa kwenye viambishi nya ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa. Mwanafunzi anapokitumia kiambishi hiki hana budi kuteua kiambishi cha ngeli kinacholeta uwiano wa upatanisho. Mwanafunzi akitumia kiambishi kisichofaa atakuwa amevunja kanuni za kisarufi. Kwa mifano:

35. (i) a*. Tulikula chakula na tukaelekea chumba ya kulala.
(i) b. Tulikula chakula na kuelekea chumba cha kulala.
(ii) a*. Niliota mvua wa ladi na umeme inanyesha.
(ii) b. Niliota mvua ya radi na umeme inanyesha.
(iii) a*. ----- vitambaa za kutandika viti za wageni.
(iii) b. -----vitambaa nya kutandika viti nya wageni.

Kwa kawaida ‘-a’ unganifu hutumiwa na kiambishi cha ngeli pamoja na nomino kuunda kivumishi. Vivumishi hivi huundwa kwa kiambishi ‘-a’ ambacho ni cha tamati kinachoambatishwa kwenye viambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno. Kwenye mifano iliyo hapo juu wanafunzi walikosa kuambatanisha kiambishi kifaacho, hawakuzingatia viambishi nya ngeli ya nomino husika.

4.2.4 Ukiushi wa viambishi vipatanishi vya hali ya udogo na ukubwa.

Katika lugha ya Kiswahili nomino huweza kuwa katika hali ya wastani (kawaida), ukubwa au udogo. Nomino ikitumiwa katika hali ya ukubwa hurejelea maumbile yenyewe ukubwa usio wa kawaida. Hurejelea pia sifa zisizo za kawaida. Kuhusu upatanisho wa kisarufi pamoja na ngeli, nomino katika hali ya ukubwa huchukua viambishi vya ngeli ya LI- YA-. Licha ya kuwa nomino huweza kubadilika ili kuonyesha ukubwa, nomino pia hubadilika ili kuonyesha udogo. Nomino ikitumiwa katika hali ya udogo hurejelea maumbile yenyewe udogo usio wa kawaida. Huweza pia kudokeza dhana ya dharau. Upatanisho wa kisarufi pamoja na ngeli hubainika kwa matumizi ya viambishi vya ngeli ya KI- VI-. Nomino ambazo zimeandikwa katika hali ya ukubwa au udogo hubadilisha upatanisho wa ngeli ya awali na kuingia katika ngeli ya LI-YA- na KI- VI- mtawalia. Baadhi ya mifano iliyokiuka upatanisho huu ni:

36. (i) a*. Nilipokipitisha kichwa changu kwenye ako kidirisha kadogo-----
(i) b. Nilipokipitisha kichwa changu kwenye hicho kidirisha kidogo-----
(ii) a*. Jitu huyo pamoja na wenzake waliingia ----- jitu aliniuliza-----
(ii) b. Jitu hilo pamoja na wenzake waliingia-----jitu liliniuliza-----

Wanafunzi walikosa kung'amua kuwa nomino inapoandikwa katika hali ya ukubwa, kiambishi cha upatanishi huwa kinabadilika na kuwa cha ngeli ya LI- YA-. Waliandika 'jitu aliniuliza' badala ya 'jitu liliniuliza', 'jitu huyo' badala ya 'jitu hilo'. Kwa sababu wao wanajua nomino jitu ni ukubwa wa nomino mtu inayopatikana katika ngeli ya A- WA-, kwa kufikiria kwao bado nomino hiyo inabakia katika ngeli ya A- WA- hata baada ya kubadilishwa na kuwa katika hali ya ukubwa. Isitoshe, lugha ya kwanza pia ilichangia katika baadhi ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Hii ni kwa sababu wakati mwanafunzi anapojieleza katika lugha ya Kiswahili, atarejelea kanuni zinazopatikana katika lugha ya

Ekegusii anayoifahamu vizuri. Mwanafunzi atahamisha kanuni za lugha ya Ekegusii hadi Kiswahili. Kwa mfano, mwanafunzi aliandika ‘ako kidirisha kadogo’ badala ya ‘hicho kidirisha kidogo’ kwa sababu katika lugha ya Ekegusii, kiambishi cha udogo ni { ka-/ ga- } ilhali katika Kiswahili sanifu kiambishi cha udogo ni {ki-} au {kiji-}. Katika lugha ya Kiswahili kiambishi {ki-} hutumiwa katika maneno yaliyo na silabi zaidi ya mbili. Kwa mfano: ‘dirisha’ katika hali ya udogo inakuwa ‘kidirisha’. Maneno yaliyo na silabi mbili huchukua viambishi {kiji}. Mfano: ‘mtu’ inabadilika na kuwa ‘kijitu’. Ikumbukwe kuwa nomino zilizo na mianzo ya ‘ki’ huchukua kiambishi {kiji} hata kama nomino hizo zina silabi zaidi ya mbili. Mfano, ‘kikombe’ itakuwa ‘kijikombe’.

4.2.5 Ukiushi wa viambishi vipatanishi vya ngeli

Makosa haya hutokea pale ambapo upatanisho wa kisarufi haujazingatiwa. Mwanafunzi anapoteua kiambishi kipatanishi kisichofaa huwa amefanya kosa la kisarufi. Ili mwanafunzi aweze kutunga sentensi sahihi zinazofuata kanuni za kisarufi za Kiswahili Sanifu sharti atue kiambishi kipatanishi kinachowiana na maneno mengine katika sentensi. Kwa mfano:

37. (i) a*. Tukiwa kule angani niliota kuwa ndege amepotesa mwelekeo.
(i) b. Tukiwa kule angani niliota kuwa ndege imepoteza mwelekeo.
(ii) a.* Mambo mengi itafanyika-----
(ii) b. Mambo mengi yatafanyika-----

Mifano hii imedhihirisha kuwepo kwa makosa ya ukiushi wa vipatanishi. Mwanafunzi hana budi kuteua kiambishi kipatanishi sahihi ili aweze kutunga sentensi sahihi zinazofuata kanuni za kisarufi za Kiswahili sanifu. Uteuzi wa vipatanishi hutegemea jinsi

nomino husika ilivyoainishwa. Nomino inapoainishwa katika ngeli fulani, hutumia vipatanishi vya ngeli hiyo. Kwa mfano, nomino ndege imeainishwa katika ngeli ya A-WA- badala ya kuainishwa katika ngeli ya I- ZI-. Ndiyo sababu mwanafunzi akaandika “---ndege amepoteza mwelekeo.” Ukweli ni kuwa nomino hii ina maana zaidi ya moja. Kuna ndege ambaye ni kiumbe mwenye mabawa na manyoya anayeruka angani na ambaye pia huitwa nyuni. Kutokana na maelezo haya nomino hii itachukua viambishi vipatanishi vya ngeli ya kwanza. Maana ya pili ya nomino hii ni chombo cha kusafiria angani; pia huitwa eropleni. Kutokana na muktadha ambao mwanafunzi alitumia nomino hii alimaanisha maana ya pili; ndege chombo cha kusafiria wala sio kiumbe kwa hivyo angetumia kipatanishi I- ZI-.

4.2.6 Matumizi mabaya ya vihusishi

Kihusishi ni neno au fungu la maneno ambalo huonyesha uhusiano baina ya kitu na kingine au mtu na mwingine. Uhusiano huu unaweza kuwa wa mahali, wakati au kiwango. Mifano ya makosa yaliyotokana na matumizi mabaya ya vihusishi ni :

38. (i) a*. Muda si muda lile jitu likanishika kwa mkono na kukimbilia kwenda msituni katika majitu wenzake.
 - (i) b. Muda si muda lile jitu lilinishika mkono na kukimbia msituni kwa majitu wenzake.
 - (ii) a*. Nilipokuwa nikipita katika kichorochoroni kimoja-----
 - (ii) b. Nilipokuwa nikipita katika kichorochoro kimoja----- Au
 - (ii) c. Nilipokuwa nikipita kichorochoroni kimoja-----

Vihuishi ‘katika’ na ‘ndani ya’ ni vya mahali vinavyoonyesha uhusiano wa mahali. Vinapotumika katika sentensi vinaashiria mahali maalum. Mwanafunzi anapovitumia kwa pamoja katika sentensi moja kurejelea mahali fulani huwa anafanya kosa. Inafaa kukitumia kihuishi kimoja tu.

4.2.7 Matumizi mabaya ya viunganishi

Kiunganishi ni neno au fungu la maneno linalounganisha mafungu mawili ya maneno au sentensi mbili. Kuunganisha huku huwa kusudi la kutoa maana fulani kama vile: kuleta dhana ya kujumlisha, kuleta dhana ya kukataa kwa kusudi la kupambanua, kuleta dhana ya chaguo au kuonyesha sababu au masharti. Makosa yaliyojitokeza katika sehemu hii yalihusu kutumia kiunganishi kisichofaa au kutotumia viunganishi mahali kulipostahili. Kwa mfano:

39. (i) a*. Bali ni kwa hii arusi ilikuwa ya bi. arusi na Bw. arusi nao walikuwa kaka yangu na dada yangu.
 - (i) b. Pamoja na hii arusi iliyokuwa ya Bi. na Bw. arusi waliokuwa ndugu zangu.
 - (ii) a*. Siku hiyo nilirauka asubui na mapema fauka ya maandalizi ya arusi.
 - (ii) b. Siku hiyo nilirauka asubuhi na mapema kwa minajili ya maandalizi ya arusi.
 - (iii) a*. Siku hiyo ilionekana kuwa njema alakini haikuwa vile nilivyodhani.
 - (iii) b. Siku hiyo ilionekana njema lakini haikuwa nilivydhani.

Mwanafunzi anapaswa kuelewa kuwa anapotumia viunganishi katika kuunganisha fungu la maneno au sentensi lazima dhana iliyokusudiwa ieleweweke. Kutokana na mifano iliyo

hapo juu mwanafunzi alishindwa kuelewa dhana zinazowakilishwa na viunganishi hivyo. Kiunganishi ‘bali’ huleta dhana ya kukataa kwa kusudi la kupambanua. Pia kiunganishi ‘fauka ya’ huleta dhana ya kujumuisha lakini kile mwanafunzi alichokikusudia ni kuonyesha sababu. Kwa hivyo angetumia kiunganishi ‘kwa minajili’. Mwanafunzi ametumia neno ‘alakini’ badala ya kiunganishi ‘lakini’. Sababu ya kutokea kwa makosa haya ni kutolewa dhana tofauti zinazowasilishwa na viunganishi mbalimbali.

Sababu nyingine ya makosa haya kutokea ni ujumlishaji mno. Ujumlishaji mno ni kule kutumia mikakati ya kujifunza ambayo tayari ipo katika hali tofauti na pale ambapo inastahili kutumiwa. Anayejifunza lugha hujumlisha sheria tofauti mahali ambapo haifai na kusababisha makosa. Aghalabu mwanafunzi huwa na uelewa wa kanuni zinazopatikana katika lugha lengwa lakini huzitumia kwa njia isiyofaa. Wanafunzi wanaelewa kuwa nomino za lugha ya Kiswahili zina umoja na wingi, hivyo kuna wale wanaoambisha nomino zisizokuwa na wingi na viambishi ambavyo wanadhani ni sahihi. Mathalani, ngeli ya tisa (I-ZI-) haina viambishi vyta wingi lakini wanafunzi waliandika baadhi ya nomino zinazopatikana katika ngeli hii kwa wingi.

4.2.8 Matumizi mabaya ya virejeshi

Virejeshi ni viambishi ambavyo huturejesha kwa mtendaji au yambwa na kumtambulisha zaidi. Ikiwa ni kitu ambacho hakina nafsi virejeshi huwa na dhima ya kutubainishia kinachorejelewa ni nini. Baadhi ya makosa wanafunzi walifanya ni kutumia virejeshi visivyofaa na kwingine wakakosa kutumia virejeshi pale vilipohitajika.

Kwa mfano:

40. (i) a*. Jambazi mwenye alikuwa ameiba ametoroka.
(i) b. Jambazi aliyeiba alitoroka.
(ii) a*. ----- watu watatu asiyofahamu waliingia ndani ya nyumba.
(ii) b ----- watu watatu asiwafahamu waliingia ndani ya nyumba.

Katika mfano wa kwanza mwanafunzi ametumia kivumishi cha pekee ‘mwenye’ badala ya ‘o’ rejeshi ‘ye’. Hivyo amekosa kutumia kirejeshi ingawa alitakiwa kukitumia. Katika mfano wa pili kirejeshi kilichotumiwa hakiambatani na ngeli ya nomino husika. Nomino husika iko katika hali ya wingi kwa hivyo mwanafunzi angetumia kirejeshi ‘o’ badala ya ‘yo’.

4.2.9 Ukiushi wa viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi

Kunyambua kitenzi ni kukirefusha kwa kukiongezea viambishi katika mzizi. Kitensi kinaponyambuliwa maana tofauti tofauti hubainika. Hata hivyo kategoria ya neno haibadiliki. Maana ya kimsingi ya kitensi hubakia vile vile. Ilibainika wazi kuwa kuna baadhi ya wanafunzi hawajui kunyambua vitenzi katika hali tofauti tofauti. Wanafunzi walifanya makosa katika kauli mbalimbali. Kwa mfano:

41. (i) a*. Alianza kuniambia kuwa mimi nimemfurahiza.
(i) b. Alianza kuniambia kuwa mimi nimemfurahisha.
(ii) a* Nilipochelewa kufika nyumbani niligofya ambalo nitafanyiwa na wazazi wangu.
(ii) b. Nilipochelewa kufika nyumbani niliogopa nitakalofanyiwa na wazazi wangu.

Katika mifano hii wanafunzi wamenyambua vitenzi vibaya. Katika sentensi ya pili mwanafunzi amenyambua kitenzi ‘ogopa’ katika kauli ya kutendesha badala ya kauli ya kutenda. Makosa haya ya mnyambuliko yalijitokeza katika kauli tofauti tofauti.

4.2.10. Ukiushi wa viambishi vya njeo na hali.

Njeo hueleza uhusiano uliopo baina ya wakati wa kutamka na wa kutenda jambo. Hali nayo hutumika katika vitenzi kuonyesha muda au kipindi maalumu ambamo tendo fulani lilifanyika huonyesha kukamilika, kutokamilika au kuendelea kwa tendo. Wanafunzi hutatizika wanapotumia njeo na hali katika kazi zao. Viambishi vinavyoashiria njeo na hali huchanganywa kiasi kwamba wakati uliokusudiwa haubainiki wazi hivyo basi kuleta utata katika kazi husika. Mifano ya makosa yaliyojitekeza katika kazi za wanafunzi :

42. (i) a*. Nilipoona jitu hilo nilishindwa nitakimbilia wapi.
(ii) b. Nilipoona jitu hilo nilishindwa ningekimbilia wapi.

Kiambishi ‘-ta’ hutumiwa kuonyesha wakati ujao. Kulingana na muktadha wa sentensi hii wakati unaozungumziwa ni wakati uliopita. Kiambishi kinachotumiwa kuashiria wakati uliopita ni ‘li’. Katika sentensi hii mwanafunzi amechanganya kiambishi cha wakati uliopita na wakati ujao na kuzua utata.

4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumechangana makosa ya kisintaksia yanayojitekeza katika kazi za wanafunzi. Tumeonyesha jinsi yamedhihirika katika kazi za wanafunzi walizoziandika.

Kutokana na makosa haya ni thibitisho kuwa wanafunzi wameathirika pakubwa sana na lugha yao ya kwanza. Tumeeleza visababishi nya makosa haya na kutoa maumbo sahihi ya maneno pamoja na tungo. Kijumla katika sehemu hii makosa mengi yalijitokeza katika sehemu ya kirai-tenzi kwa sababu ya kitende cha Kiswahili kina uwezo wa kuchukua viambishi tofauti vinavyowakilisha dhana mbalimbali. Vilevile, makosa haya yalitokea wakati kirai-nomino na kirai-tenzi vilipounganishwa hivi kwamba baadhi ya viambishi nya upatanisho vilivyoambishwa katika kitende havikufungamana na nomino au kiima cha kirai-nomino. Kwa kuchunguza makosa haya ni dhahiri kuwa wanafunzi wanafanya makosa kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisumu ya lugha yao ya kwanza na kuilazimisha mifumo hiyo katika lugha ya Kiswahili. Isitoshe, makosa haya yametokana na ujumlishaji mno wa kanuni za lugha yao ya kwanza. Aidha, makosa mengine ni ya kufundishwa lugha kwa njia isiyofaa, baadhi ya walimu ni wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii, wana utendaji mbaya katika uzungumzaji na hili huathiri wanafunzi wao.

Tumeyachanganua makosa haya na kueleza visababishi nya makosa hayo katika mifano mahsus. Ni vyema kuzungumzia sababu zinazosababisha kutokeea kwa makosa haya kwa kijumla bila kujikita katika mifano mahsus. Kwa mujibu wa Ellis (1985, 1994), nadharia ya isimu hutuwezesha kueleza aina ya makosa yanayofanywa kwa kulinganisha lugha ya anayejifunza lugha ya pili na lugha lengwa. Nadharia ya isimu hutuwezesha kueleza jinsi ambavyo mwanafunzi amekiuka kaida za lugha lengwa. Udhaifu wa nadharia hii haituambii ni kwa nini mwanafunzi anafanya makosa hayo.

Watafiti kama Ellis (1994) wameeleza sababu zinazosababisha makosa kutokeea kwa wale wanaojifunza lugha ya pili. Baadhi ya sababu ambazo wameeleza zina mwingilio na zile ambazo tumezitaja katika sehemu ya uchanganuzi wa makosa lakini tumeona ni

vyema kutaja sababu kwa kijumla bila kujikita katika lugha mahsus. Sababu ya kwanza ni kutojua mipaka ya sheria au kaida za lugha anayejifunza. Mwanafunzi hutumia sheria bila kujuu jinsi inapaswa kutumiwa. Aghalabu mwanafunzi huwa amefunzwa kanuni za lugha anayejifunza lakini kwa kuwa hajazimudu vyema yeze huzitumia hapa na pale bila kuwa na uelewa wa kuzitumia.

Lugha ya kwanza huchangia kutokea kwa makosa hayo kwa sababu mwanafunzi anaposhindwa kujieleza katika lugha lengwa, atarejelea lugha anayoifahamu vizuri ambayo ni lugha ya kwanza. Mwanafunzi huhamisha dhana kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Ndiposa utapata kuwa makosa yanayofanywa hufanana na mifumo ya lugha ya kwanza. Makosa mengine huonekana kama tafsiri ya moja kwa moja kutoka lugha ya kwanza. Sarufi ya lugha ya kwanza huwa msingi wa sarufi ya lugha ya pili. Mwanafunzi atatumia sarufi tayari anailewa akiendelea kujifunza sarufi ya lugha lengwa.

Sababu nyingine ni kutotumia sheria kikamilifu. Mwanafunzi hutumia sheria zilizo rahisi kuwasiliana, mwanafunzi hujua hata kama hatafuata kanuni sahihi kuwasiliana ataeleweka. Mwanafunzi anaweza kueleweka kwa kutumia sehemu ya sheria hivyo kuendelea kufanya makosa bila kujali. Mwanafunzi hujifunza sheria ambazo zitamsaidia katika harakati za kuwasiliana. Tujuavyo jinsi mtu anavyowasiliana ndivyo anavyoandika kwa hivyo atahamisha makosa yale ayafanyayo wakati wa mawasiliano na kuyapeleka katika maandishi.

Sababu nyingine ni ugumu wa kujifunza lugha. Kuna mifumo mingine ya lugha inayowatatiza wanaojifunza lugha. Lugha huwa tofauti na lugha nyingine, mwanafunzi anapojifunza lugha iliyotofauti kabisa na lugha yake ya kwanza hupata shida sana.

Ikumbukwe kuwa tayari mwanafunzi huyu amejifunza mifumo ya lugha ya kwanza kwa hivyo itakuwa vigumu kwake kuanza kujifunza mifumo iliyotofauti ya lugha ya kwanza. Tayari akilini mwake amemudu mifumo ya lugha ya kwanza anayoitumia kila siku katika mawasiliano. Kuna makosa mengine yalitokana na sifa ya ubia. Kama tulivyotaja hapo awali kuwa makosa hujitokeza katika viwango vyote vya usomi, jambo hili ni kweli. Tofauti ni kuwa kiwango cha makosa wayafanyao ni tofauti. Kwa kijumla tumetaja sababu zinazokisiwa kusababisha makosa haya.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulinuia kuchanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii wanapojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili. Sura ya kwanza ni muhtasari wa jinsi utafiti ulivyofanywa. Imeshughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia na njia za utafiti. Katika sura ya pili tumeainisha fonimu za lugha ya Ekegusii na Kiswahili na kuchambua miundo ya silabi za lugha hizi. Tumepata kuwa mifumo ya fonimu za lugha hizi mbili ni tofauti. Kutokana na tofauti hii wanafunzi huathirika pakubwa sana wanapotumia lugha ya Kiswahili. Katika sura ya tatu na nne tumechananua data kwa misingi ya hatua tano alizozipendekeza Corder (1974). Makosa mengi yaliyojitokeza yalitokana na athari za lugha ya kwanza. Katika sura hizi tumechananua data tuliyokusanya kwa njia ya insha zilizoandikwa na wanafunzi. Insha zilikuwa za wanafunzi walio katika viwango viwili tofauti vyatya usomi.

5.2 Hitimisho

Utafiti huu ulikuwa unachanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa athari za L1 kwa matumizi ya Kiswahili kama L2. Kutokana na utafiti huu, nadharia tete zetu zimedhihirishwa kuwa na mashiko. Tulidai kuwa makosa ya kifonolojia,

kisintaksia na miundo ya maneno katika Ekegusii ni tofauti na ile ya lugha ya Kiswahili. Haya yamejitokeza wazi kutokana na data tuliyokusanya inayothibisha kuwepo kwa makosa mengi ya kategoria za kisarufi. Aidha, tumeainisha fonimu za Kiswahili Sanifu na Ekegusii na kuonyesha fonimu zinazopatikana katika kila lugha na kuonyesha tofauti iliyoko kifonimu inavyochangia kuwepo kwa makosa mengi ya kifonolojia.

Imejitokeza kuwa makosa yanayotokea katika insha za wanafunzi hutokea katika viwango vyote vya usomi. Makosa haya yanaendelea kupungua kadiri mwanafunzi anavyoendelea katika viwango vya juu vya usomi. Imebainika wazi kuwa wanafunzi hufanya makosa haya kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisimu ya L1 kwenda kwa L2. Mathalani lugha ya Ekegusii haina fonimu /l/ na kwa hivyo mwanafunzi anapoandika neno kama /lala/ hutumia fonimu inayopatikana katika lugha yake ya kwanza. Hivyo ataandika /rara/ badala ya /lala/. Makosa haya yamekiuka kanuni za kifonolojia za Kiswahili sanifu. Lakini ikumbukwe kuwa makosa haya hayawi kizuizi cha ujifunzaji lugha bali ni harakati za mtu kuimudu L2. Kutokana na matokeo haya ni dhahiri kuwa mwanafunzi hawezikupata umilisi asilimia mia moja, kwa sababu wanafunzi hawa si wazawa wa lugha ya Kiswahili. Hivyo hawawezi kufikia umilisi wa juu zaidi. Watakalofanikiwa ni kupunguza makosa haya kadiri wanavyoendelea kwenye viwango vya juu zaidi.

Nadharia ya Uchanganuzi makosa imetufaa katika utafiti huu. Tumefuata hatua za nadharia hii katika kuchanganua data. Tumeyaainisha makosa hayo katika kategoria na tumeeleza visababishi vya makosa hayo kisha kutoa maumbo sahihi.

Utafiti huu umebaini chanzo cha matokeo mabaya katika somo la Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Hata kama kumewepo na tetesi kuwa wanafunzi hawafanyi vyema katika somo hili hakuna tafiti za kutosha ambazo zimefanywa ili kutatua tatizo hili.

Kwa kweli kutokana na matatizo haya wanafunzi hufanya vibaya katika mitihani ya kitaifa na haya huchangia matokeo duni kijumla .

5.3 Mapendelezo

Katika sura hii tumetoa mapendelezo yatakayowasaidia walimu wa lugha ya Kiswahili kuongoza wanafunzi wao kupunguza makosa yanayojitokeza katika kazi zao. Tungependelezo walimu watumie mtazamo wa uchanganuzi linganuzi katika kulinganua lugha zinazohusika. Itakuwa rahisi kutambua ugumu ambao wanafunzi wanakabiliana nao. Ikiwa mwalimu atatambua vipengele vya lugha vinavyotatiza mwanafunzi, anaweza kumwelekeza mwanafunzi jinsi ya kutatua ugumu. Mwanafunzi anafaa kuelewa kuwa lugha hutofautiana kiisimu, kwa hivyo wasifikirie kwanza katika lugha yao ya kwanza ndiyo watafsiri kwenda lugha lengwa. Wanafunzi wanafaa kujifunga katika lugha lengwa na kufuata kanuni zake.

Wanafunzi wahimizwe kutumia Kiswahili sanifu wanapowasiliana kwa sababu lugha ya mazungumzo inaathiri mno lugha andishi, hivyo kuna uwezekano kuwa wakijieleza barabara katika mazungumzo huenda wakapunguza makosa yanayojitokeza katika kazi andishi. Walimu nao watumie maelezo na alama mahsusini za usahihishaji wa insha. Mara nyingi wanafunzi hawaelewi wanapofanya kosa, kwa sababu kazi husahihishwa bila alama au maelezo ya kumwelekeza mwanafunzi. Ni muhimu mwalimu kuwa na njia mwafaka ya kukosoa insha za wanafunzi. Mathalani, ikiwa kosa ni la kisarufi lipigiwe vijistari viwili chini yake na lile la tahajia lipigiwe kijistari kimoja. Kisha mwalimu anafaa kuwaelekeza wanafunzi kujua ni makosa yepi ya sarufi na ni yepi ya tahajia. Pia anafaa kutoa marejeleo ya vitabu vinavyoshughulikia vipengele vinavyowatatiza wanafunzi.

Mapendekezo zaidi ni mwalimu kurudia dhana ambazo wanafunzi hawakuelewa vyema. Uchanganuzi makosa utamfaa mwalimu kwa sababu atajua vipengele vyta lugha ambavyo vinastahili kutiliwa mkazo kulingana na uzito wa makosa na kuamua ni viyi vitashughulikiwa. Urudiaji huu wa kufunza vipengele vinavyowatatiza wanafunzi huwasaidia kuwa na umilisi wa lugha ufaao katika lugha.

Tungependekeza walimu waweze kuweka msingi thabiti kuanzia madarasa ya chini ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na umilisi mwafaka wa lugha hii mapema. Msingi bora wa fonimu utawawezesha wanafunzi kuelewa tofauti iliyoko kifonimu baina ya lugha mbili na hili litawawezesha kuimudu lugha hii mapema. Isitoshe, upungufu na ukosefu wa vifaa bora vyta mafunzo vimechangia matatizo haya, kwa hivyo tunapendekeza kuwepo na vifaa vyta kutosha vyta kufunzia wanafunzi. Aidha wakuza mitaala hawakizingatia kuwepo kwa lugha tofauti nchini Kenya. Wao walichukulia kuwa lugha zote ni sawa na wanaojifunza L2 hutatizika sawa. Mitaala ilikosa kuonyesha tofauti za kiisumu kati ya lugha asilia na jinsi inavyoathiri ujifunzaji lugha, ingekuwa vyema ikiwa mitaala ingebainisha tofauti hizi na athari za kila lugha asilia katika ujifunzaji wa L2.

Utafiti huu haujashughulikia matatizo yote yanayoikumba lugha ya Kiswahili kwa sababu muda ulikuwa mfupi. Tungependekeza utafiti ufanywe kubainisha kama makosa haya yana ubia wowote, kila anayejifunza lugha ya pili hufanya makosa sawa. Kwa minajili ya tafiti za siku za usoni, makosa zaidi huenda yakapatikana iwapo sentensi zilizoandikwa zitatumwi badala ya wanafunzi kuandika insha waandike imla. Aidha data inaweza kukusanya kuitia kanda za kunasia sauti ili kujua ni viyi wanafunzi wanavyotumia lugha katika maongezi. Tafiti zingine zifanywe kuchanganua matatizo haya kwa kina hasa yale ya kisemantiki. Utafiti mwingine ufanywe kutafuta njia ya kusuluhisha makosa haya na pia uweze kuangazia ni kwa kiwango kipi makosa haya yanaathiri utendaji wa wanafunzi na umilisi wao wa lugha

ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kuwa wakuza mitaala watayatambua matatizo yanayowakabili wanafunzi wa lugha ya Kiswahili na kutafuta mbinu za kuyatatu.

MAREJELEO

Corder, S.P. (1967) *Error Analysis and Interlanguage*, Oxford: Oxford University Press.

_____(1981) *Error Analysis*, London: Longman.

_____(1973) *Introducing Applied Linguistic*.Harmondsworth: Penguin Books.

Crystal, D. (1991) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. New York : Bluckid Publisher.

Ellis, R.(1985) *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: OUP.

- _____(1994) *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford: OUP.
- Gass, S. na L. Selinker (2008) *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. New York, Routledge.
- Gesare, (1992) *Mofolojia ya Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya M.A. (UON)
- Guthrie, M. (1948) *Classification of Bantu Languages*. Oxford. Oxford University press.
- Habwe, J. H. na P. Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers
- Iribemwangi, P. (2008) *A Sychronic Segmental Morphophonology of Standard Swahili*. Unpublished PhD Thesis. UON.
- _____(2010) *The Structure of Swahili; Sound Changes and Words*, saarbrucken; VDM Verlag.
- Jonhstone, H. W. (1919) *A Comparative Study of the Bantu and Semi-Bantu Languages*. London: Oxford University Press.
- Katamba, F. (1992) *An Introduction to Phonology*. London: Longman.
- Kihore, Y. M. et al (2003) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI
- Komenda, S. (2011) *An Autosegmental Analysis of Vowel Compensatory Lengthening in Ekegusii*. Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta University.
- Massamba, D. P. (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* Dar es Saalam: TUKI.
- Mbula, J. (2011) *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kikamba wanapoijifunza Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya M.A. (UON).
- Mgullu, R. S. (1999) *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publisher

- Mutugu, (2001) *Makosa ya Kileksia katika Insha za Wanafunzi wa Kidato cha kwanza*. Tasnifu ya M.A. (UON)
- Mwaniki, N. I. (2000) *A syntactic Study of the Interlanguage of Kikuyu Learners of English. A Second Language*. PhD.Thesis. Nairobi: UON.
- Nyakundi, P. M. (2010) *Motivation, Morphological Process in Egesembesa Argot Ekegusii-speaking Males of Western Kenya*. Unpublished MA Thesis, Kenyatta University
- Osinde, K. N. (1988) *A morphosyntactic Analysis of Ekegusii*.Tasnifu ya M.A.(UON)
- Otiende, M. A. (2013) *Athari za Mofofonolojia ya Kibasuba katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya pili*.Tasnifu ya M.A. (UON).
- Polome, E. C. (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.
- Rapando, M. M. (2005) *Makosa ya Kimofosintaksia Yanayojitokeza katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi*. Tasnifu ya M.A (UON).
- Radford, (1997) *Syntactic Theory and the Structure of English: A minimalist Approach*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Selinker, L. (1969) *Language Transfer, General Linguistics*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).
- _____ (1972) *Interlanguage*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).
- TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam : Educational publishers and Distribution LTD.
- Yule, G. (1996) *The Study of Language* (2nd ed.), UK. Cambridge University Press.